
JUNI MMXXV - TOLEO LA XLIV

# NGURUMO
*ya Mwandishi*




**HABARI KUU:**

**Watanzania Tena!**
**Safal Cornell Kiswahili Prize**

## YALIYOMO

**TAHARIRI— Uk 02**
TUTAFIKA TUNAPOPATAKA

**MWANDISHI WETU— Uk 03**
SABRINA HASSAN LIGANGA 'SABRA'

**NEW IN TOWN: Uk 04**
MTUHUMIWA, MKWE WA JAJI MKUU

**PITIO LA VITABU— Uk 05**
KILIO CHETU '3'

**SAIKOLOJIA: Uk 06— 07**
SAIKOLOJIA YA MALEZI KWA VIJANA

**MAKALA: Uk 08 - 09**
FASIHI ITATUFIKISHA TUNAPOTAKA?

**KUTOKA KWA FANANI: Uk 10—11**
SALUM MAKAMBA ATUFUNZA

**RIWAYA: Uk 12—13**
MSALITI '5'

**RIWAYA: Uk 14—15**
Najutia Kuwa Na Wewe '4'

**YA KALE NI DHAHABU: Uk 16**
Alibaba na Wezi 40 '20'

**HABARI MOTO: Uk 17**
WATANZANIA WANG'ARA TENA

**SHUBAKA LA VITABU: Uk 18**
HISTORIA YA VITABU

**KITABU NILICHOSOMA: Uk 19**
MPATANISHI

**MATANGAZO: Uk 20**

**MALENGA WA KILEO: Uk 21**

**HABARI PICHA: Uk 22**

**KUTOKA MAKTABA: Uk 23**
Maisha ni Mapambano '10'

**ELIMU JAMII: Uk 24 - 25**
SAFARI YA MALEZI— 2

**HADITHI: Uk 26 - 27**
Happy New Year '7'

**HADITHI: Uk 28 - 29**
NGUVU YA KIAPO '02'

## TAHARIRI:

# TUTAFIKA TUNAPOPATAKA

Wasalaam!

Hakika tutafika tunapopataka. Hili ni toleo la 44 la jarida letu pendwa la kifasihi la Ngurumo ya Mwandishi.

Hakika, kila mmoja wetu akitazama mbele, mbele kabisa ya upeo macho yake, hushindwa kuona sawasawa kile anachokio na. Anajikuta anapata tabu kidogo au sana kufananisha anachokiona na kile anachofikiri.

Ukiweza kufananisha unachokiona na kile unachofikiri basi ujue ndoto yako inakaribia kuwa kweli. Lakini hata kama hu jaweza, usikate tama, maana, asubuhi moja lakini kila mtu huamka kwa upande wake.

Tutafika tunapopataka tu ikiwa tutaweka juhudi katika kila kitu tunachofanya. Juhudi, I ndani yetu wenyewe, kinachotakiwa kufanyika ni kuitoa kutoka ndani na kuiweka matendoni ili izae matunda.

Kaza macho, tazama mbele, nyanyua mguu piga hatua. Mafan kio yako utayapata wewe mwenyewe kwa juhudi zako na si kul etewa na mtu.

Soma vitabu, shiriki semina na warsha, jifunze kupitia wengine, usiwe mchoyo wa maarifa. Na ukifanikiwa, usiwasahau uli yowaacha nyuma.

Upendo ndiyo kila kitu katika maisha!

*R.R Mwambe*
0766974865

**NGURUMO YA MWANDISHI**


**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

## MWANDISHI WETU:
## SABRINA HASSAN LIGANGA 'SABRA'

**Kwenye Safu ya Mwandishi Wetu toleo hili la 44, tunamsogeza kwenu Sabrina Hassan Liganga au kama anavyojulikana kwa lakabu yake SABRA.**

**Yeye ni miongoni mwa waandishi mahiri wa hadithi kwenye mitandao ya kijamii, hususani Facebook.**

**Sabra ni nani? Na anafanya nini? Na anautazama vipi uandishi?**



**Sabrina Hassan Liganga**

**Mwandishi wa Hadithi Mtandaoni**

Jina langu ni Sabrina Hassan Liganga. Lakini nafahamika kwa jina la Sabra wa Abdullah, hilo ndilo jina langu la kiuandishi na ndilo maarufu.

Nimezaliwa Wilaya ya Kisarawe Mkoa wa Pwani, nikaanza kusoma huko katika Shule ya Maingi Chanzige, lakini nilipofika darasa la tano nikahamishwa shule na kuchukuliwa na mama na kwenda kuishi Kibiti kwani kwa wakati huo wazazi wangu walikuwa wametalikiana.

Nilipofika Kibiti niliendelea na masomo na kufanikiwa kumaliza elimu ya sekondari mwaka 2012 katika shule ya sekondari iitwayo Msafiri.

Nikiwa shule nilikua napenda sana kutunga na kuandika hadithi kwenye daftari. Nilikua nafanya hivyo kwa kujifurahisha tu lakini baadae ndipo nikagundua naweza kufanya kitu na kweli ikawa hivyo.

Hapo mwanzoni nilikua najishughulisha na shughuli mbalimbali. Mara wakala, mara machinga, lakini hivi sasa inafika hata miaka miwili nipo tu nyumbani.

Kwakweli, mpaka sasa nimeandika riwaya kumi na mbili.

Sijafanikiwa kuchapa kitabu hata kimoja. Niseme tu kwasababu sijaamua maana hakuna kipingamizi chochote cha kunizuia kufanya hivyo.

Changamoto ninazokutana nazo ni muda. Nakosa muda mzuri wa kuandika kwasababu mimi ni mke na ni mama wa watoto watatu. Majukumu ya nyumbani na ya kifamilia ni mengi hivyo nakosa muda mzuri wa kutuliza akili na kufanya uandishi.

Mimi kama wengine, nina ndoto, na moja ya ndoto yangu ni kukutana na watu mashuhuri walio katika tasnia hii ya uandishi ili niweze kupata mawili matatu kutoka kwao na kuzidi kujifunza.

Nawashauri wasichana wenzangu wasikate tamaa. Wajiwekee malengo madhubuti ili kufikia kwenye kilele cha ushindi. Kuandika kuna raha yake, na ukizoea kuandika hautatamani kuacha.

Kwa wasomaji wangu nawasihi waendelea kuniunga mkono japokuwa kuna muda huwa nakuwa kimya kwa kipindi kirefu bila kutoa hadithi. Nawaomba wasinitupe na waendelee kuwa na subira.

Napatikana kwenye mtandao wa facebook. Page yangu ni Sabra Stories, au Sabra wa Abdullah.

Kwa upande wa Whatsapp no yangu ni **0655471313.**

**Kama unahitaji kumsoma Bi. Sabrina, basi waweza kuwasiliana naye naye akakupatia utaratibu wa kuzipata hadithi zake. Lakini zaidi pita kwenye Facebook kwenye kurasa aliyoitaja yaani 'Sabra Stories' ili upate burudani toka kwake.**

*Hakikisha unamtembelea katika Social Media zake kama alivyojieleza ili kupata burudani murua isiyo na mawaa yoyote.*

## NEW IN TOWN :
## MTUHUMIWA, MKWE WA JAJI MKUU

**MTUHUMIWA—Hussein Tuwa**
Msichana anapojiua ndani ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam, halionekani kuwa ni jambo la ajabu sana. Ila wanapojiua wasichana wengine wawili, Jaka Brown Madega anakataa kabisa kuamini kuwa vifo vile havina uhusiano.

Udadisi wake unapoteza nguvu pale mtukutu Joakim Mwaga akibebwa na kundi la watukutu wenzake pale chuoni, anapoazimia kuangilia kati na kulivunja penzi kati yake na mrembo Moze. Lakini mtu wake wa karibu pale chuoni anapojiua katika mazingira yaleyale tatanishi, udadisi wake unaamka upya. Ndipo anapogundua siri nzito na hujuma kubwa kwa taifa, kupitia vilio vile, siri ambayo ingeweza kunusuru penzi lake na kulisambaratisha kabisa kundi halifu la vijana watukutu pale chuoni.

Kwa namna asiyoitarajia, siri aliyoibaini inapoteza maana pale anapotiwa mbaroni akiwa na maiti ya hasimu wake mkubwa, Joakim Mwaga. Tuhuma inamwangukia, mashaka yanamwandama, kusalitika kunamgubika, penzi linamponyoka na maisha yanamgeuka.

Anaionja ladha ya ukweli mchungu kuwa sio tu kwamba waridi lina mvuto wa rangi ya kupendeza na harufu nzuri pekee, bali pia lina miiba mikali.
Kinachofuata ni simanzi ya kunyong'onyeza moyo, tafrani za mfululizo, makabiliano mazito na kudiriki kusikosemekana, pale madhila yanapomkutanisha na wauaji hatari, wapelelezi wasiobahatisha… na upendo asioutarajia.

Hii ndiyo riwaya ya kwanza kabisa kuandikwa na Hussein Tuwa, na kama ulimkubali kwenye kazi zake nyingine, basi MTUHUMIWA itakuthibitishia kuwa hakika yeye amekuwa bingwa wa taharuki tangu siku ya kwanza kabisa alipoanza kuandika.




"Mtuhumiwa" ni kisa makini cha taharuki katika penzi.

**MTUHUMIWA:**
**Kinapatikana Duka la KONA YA RIWAYA Kinondoni: Simu—0655428085**
**Maduka yote ya Elite Bookshops nchini kwa Tsh 20,000 tu!**


**MKWE WA JAJI MKUU—Wilbard Makene**

Jaji Mkuu,Athumani anapata taarifa kuwa bintiye Huruma ana mahusiano ya kimapenzi na Mayunga, mtoto wa mfanyabiashara mkubwa.

Mtaani tetesi zimezagaa kwamba Mayunga ana mahusiano na watuhumiwa wa dawa za kulevya.

Athumani hapendezwi. Anatofautiana na Huruma. Inambidi Mayunga ajisafishe, huku akihatarisha maisha yake.

**MKWE WA JAJI MKUU: Kinapatikana Dar es salaam Dula la KONA YA RIWAYA: Simu — 0655428085**
**Na maduka yote ya ELITE BOOKSHOP**



# KILIO CHETU—3






**TAMTHILIYA:** KILIO CHETU
**MWANDISHI:** MEDICAL AID FOUNDATION

**MCHAPISHAJI:** TANZANIA PUBLISHING HOUSE

**MWAKA:** 1995

**JINA LA MHAKIKI:** Mwalimu Daud Makoba

***Inaendelea, sehemu ya tatu***

3. Picha na taswira

"Dubwana" –ugonjwa wa UKIMWI;

"Nguru" –aina ya Samaki wabaya–amefananishwa na mtu mbaya;

**MAUDHUI**

**DHAMIRA**

Dhamira nyingi zimejadiliwa katika tamthiliya hii, miongoni mwa dhamira hizo ni;

**i. Elimu ya jinsia na mahusiano**

Jamii imekumbwa na mmomonyoko mkubwa wa maadili pamoja na maradhi hatari yasiyotibika kama UKIMWI. Hivyo wazazi wanapaswa kuwaelimisha watoto wao juu ya njia sahihi za kujikinga na matatizo haya. Katika tamthiliya tunaona pande mbili, ule unaoshikilia ukale na upande unaotaka mabadiliko. Baba Anna, anawaelimisha watoto wake juu ya madhara ya kujihusisha na ngono katika umri mdogo, Anna anaelewa na anafanikiwa kukwepa vishawishi. Hali ni tofauti kwa Mama Suzi anaamini kuwapatia watoto elimu ya jinsia na mahusiano ni kuwaharibu na kuwapoteza. Anaposhauriwa kuwapatia watoto elimu hiyo anafoka, *"Huko si ndiko kunifundishia wanangu umalaya? Umfunze mwanangu habari za ngono…"* Kutokana na kutokukubali kuwapatia wanawe elimu hii, Suzi anapewa mimba na kuambukizwa UKIMWI.

**ii. Mmomonyoko wa maadili**

Maadili hayazingatiwi tena katika jamii. Watoto kwa wakubwa wote wamepotoka. Tunaona watu wazima *wakitembea* na watoto wadogo, mfano Chausiku ana mahusiano na mtoto mdogo Joti. Pia watoto wamejiingiza katika mahusiano ya kimapenzi, Joti ana mahusiano na Suzi. Watoto hawahawa wanaangalia video za ngono bila kuogopa chochote. Katika ukurasa wa 20 Joti anasikika akiwahamasisha wenzake.

*"Yaap, ukimtaka Suzi, chukua. Picha ya ngono, matusi angalia!"*

Mmomonyoko huu wa maadili utaondolewa endapo watoto watapatiwa elimu.

**iii. Athari ya sayansi na teknolojia**

Maendeleo ya sayansi na teknolojia yameleta mabadiliko makubwa katika jamii, mfano katika tamthiliya hii, watoto wanakwenda kuangalia picha za ngono na kuwafanya waharibikiwe kifikra kwa kutamani kuigiza kile wanachokiona. Joti, mtoto kinara wa kutazama picha hizo anaambulia UKIMWI na kufa angali mtoto mdogo.

**iv. Nafasi ya mwanamke katika jamii**

Nafasi ya mwanamke ni jumla ya mambo yote ayatendayo mwanamke katika kazi ya fasihi. Mengine huwa mazuri yanayostahili pongezi na machache huwa mabaya yanayostahili kukemewa kwa nguvu. Katika tamthiliya hii, mwanamke amechorwa kama;

- Chombo cha starehe. Mfano Joti anamtumia Suzi kwa ajili ya kujistarehesha.
- Asiyependa mabadiliko. Mama Suzi hataki kutoa elimu ya jinsia kwa wanaye.
- Asiye na maadili. Suzi hana maadili, anajiingiza katika mahusiano ya kimapenzi katika umri mdogo.
- Mwenye elimu na asiyedanganyika. Anna ana elimu ya jinsia na mahusiano, wanaume wanashindwa kumdanganya kwa pesa na maneno matamu.

*Itaendelea toleo lijalo*

## SAIKOLOJIA YA MALEZI KWA VIJANA



Madam Neema Mgao 'Psychologist'


**MALEZI YA VIJANA KUANZIA KIPINDI CHA BALEHE MPAKA MIAKA 25**

Heri ya mwezi mpya wa JULAI, nakutakia amani, furaha, mafanikio, baraka, na kukubalika nyakati zote na sehemu yoyote inayokuzunguka katika maisha yako ya kila siku. Upatwapo na tatizo lolote Mungu akupe kulitatua vizuri. KAMA NIKUOMBEAVYO WEWE NA MIMI NAJIOMBEA VIVYO HIVYO.

Katika toleo hili tuzungumzie malezi ya watoto wetu au wadogo zetu katika hatua zao mbalimbali za ukuaji. Katika matoleo ya nyuma kidogo, niliwahi kukupa hatua za ukuaji wa binadamu kulingana na umri na uhusiano wao wa kiukuaji. Ukuaji wa mwanadamu kuanzia siku 0 - kufa kwake kumegawanyika kulingana na hatua za ukuaji kadri anavyokua.

Katika toleo hili tuangazie kundi muhimu kabisa la ukuaji wa mwanadamu ambalo ni kuanzia balehe mpaka miaka 25. Mzazi au mlezi asipokua makini na kipindi hiki cha ukuaji wa mtoto hapa ndio panatengenezwa tabia ambazo ni msingi wa maisha ya mtoto huyu, hapa ndipo ambapo tutapata iwe mtu imara na shupavu au tupate mtoto au kijana ambae atakuja kuwa janga kuanzia kwenye familia mpaka kwenye jamii inayowazunguka.

Malezi ya watoto wanapofikia umri huu yaani umri wa balehe, huwa yanataka umakini sana wa mzazi au mlezi ili mtoto asiharibikiwe maishani mwake. Ni katika kipindi hiki ambapo tabia na matendo ya mtoto kwa kiasi kikubwa kinategemea sana sana kile ambacho anakiona kutoka kwa mzazi au mlezi wake. Katika hatua hii utaona kwamba kama mama au mlezi wa kike anapenda sana mapambo ya mwili basi na mtoto wa kike naye anaanza kui-



ga namna mama au mlezi anavyokua akijipamba, vivyo hivyo kwa watoto wa kiume, ni katika hatua hii ambapo mtoto wa kiume anaanza kufanya matendo sawa na ayafanyao baba yake.

Mfano: Iliwahi kutokea jambo ambalo lilihusisha ugomvi kati ya baba na mtoto/ kijana wake wa kiume. Baba alitoka na kwenda matembezini usiku na akarudi saa 8 usiku. Na tabia hiyo imekua ni tabia ya kila mara, mtoto/kijana wa kiume wa baba yule nae akaanza kutoka, ni kijana wa miaka 20. Siku moja wakagongana getini, wote wawili ndio wanarudi nyumbani. Baba anaposema asimamie nafasi yake kama baba, na aanze kumhoji mtoto alipokua, mtoto nae akasema "SASA MBONA WOTE NDIO TUNARUDI SASA HIVI?". Kwa kesi kama hiyo ukipewa nafasi ya kufanya maamuzi utafanyaje?

Ni wazi kuwa watoto hufanya yale tuyafanyayo, watoto na vijana hufanya kama vile wazazi na walezi wafanyavyo. Ni kwa asilimia chache sana hufanya mambo kwa akili zao na yale wayaonayo watu wao wa karibu wengine wakifanya. Lolote utakalofanya ni muhimu kufanya kwa weledi na kutambua kuwa unachofanya mtoto wako au kijana wako anakutazama na kujaribu kuishi vile uishivyo wewe.
Ili utuzalishie baba bora au mama bora inakupasa kufanya mambo kwa usahihi ukilizingatia hilo. Saikolojia ya binadamu yeyote yule huwa ni ya kujifunza kufanya jambo jipya kadri ya anavyolipokea na kujifunza kulitenda. Ubongo wa binadamu unajifunza na kuhifadhi jambo jipya kila iitwapo siku mpya. Ni vyema kupenyeza elimu chanya kwa mtoto au kijana wako ili imsaidie katika maisha yake.

**TABIA ZA KUZIEPUKA**
Zipo tabia ambazo zinaweza kuepukika ili mtoto au kijana asiige tabia hizo hasa tabia hasi. Kama nilivyosema kuwa, wewe wa leo ni vile ulivyoona wengine hasa walezi wako wakiishi, basi ili tumpate baba au mama bora wa kesho basi ni wewe kuishi katika misingi bora. Baba mmoja alisema, "Nimeishi na kukua katika nyumba ambayo nimemshuhudia baba akirudi amelewa, anakuja kumtukana mama usiku kucha, anampiga sana, mama alikua hajibu kitu chochote. Sasa nimekua na familia, naona kumtukana mke wangu ni jambo la kawaida".

Kumbe kama zile tabia tuzifanyazo mbele ya watoto wetu watoto wanaiga basi ni vyema tukajiepusha na tabia hasi/mbaya zote. Tabia kama ulevi kupindukia utakaopelekea kujidhalilisha au kudhalilisha wenza wetu ni tabia hasi haifai kuwepo, matusi kwa wenza wetu hayafai, kipigo kwa wenza wetu haifai mfano wa hayo na tabia zozole zile hasi, hazifai kufanywa pale tunapowaandaa watoto vijana wetu kuja kubeba majukumu baadae.
Nikutakie mafanikio na Baraka katika mwezi wote wa 7. Mungu atubariki na kutulinda sote. Amina.

**MADAME NEEMA MGAO.**
**DODOMA.**
**TANZANIA.**
**+255 763 013 206.**

# FASIHI ITATUFIKISHA TUNAPOPATAKA?

## Kuandika ni kuandika tena!

**Na Mwandihi wetu!**

Siku hizi au niseme miaka hii ya karibuni, yaani kuanzia miaka ya 2000 hivi mpaka sasa, fasihi ya Kiswahili imebuka taratibu na sasa imeshika kasi. Hili limekuja baada ya kimya kingi ambacho kwacho 'wahenga' walisema "kina mshindo mkuu".

Hakika, mshindo wake ndiyo huu sasa tunaoushuhudia. Sina uhakika sana kama ni mitandao ya kijamii iliyoletwa kupitia mapinduzi makubwa ya Sayansi na Teknolojia duniani ndiyo imekuwa chachu ya kuibua vipaji vya kifasihi vilivyojificha au ni vipi!

Lakini ninachotaka kusema ni kwamba Fasihi ya Kiswahili kufikia sasa imekuwa ni sehemu ya maisha ya vijana wengi Tanzania. Kuna wimbi kubwa la vijana ambao sasa wameamua kuitumia kalamu na kufanya sanaa adhimu ya lugha kuburudisha, kuelimisha, kukanya na kuzodoa.

Katika mazungumzo yangu na waandishi wengi wa kipindi cha sasa, naweza kuwagawanya katika makundi makubwa mawili. Lakini makundi haya, moja nalipa asilimia 80 jingine nalipa 20, kwa nini? Au kwa vipi?

Kundi kubwa la waandishi wa ki-sasa, wamedai kwamba ibuko lao la kiuandishi limechagizwa na wazazi wao kwa kuwajengea utamaduni wa kusoma tangu wakiwa wadogo labda shule ya msingi hivi. Wengi wao wamedai kwamba, wazazi wao walikuwa na hazina ya vitabu vya masimulizi anuai. Hivyo na wao walijifunza usomaji kupitia humo na baadae kujikuta wanapenda kuandika. Na baadhi yao wameweka wazi kuwa walikuwa wanaandika wakiwa shule ya msingi na kuwaburudisha rafiki zao waliokuwa wakisoma nao kwa maandiko hayo. Na sasa wengi wa hawa ni waandishi wa riwaya ambazo twazisoma kila uchao.

Kundi la pili ambalo nimelipa asilimia 20, wameweka bayana kuwa wao wamependa kuwa waandishi kutokana na kusoma kazi za watu fulani na kuwafanya kuwa 'viigizo' vyao, yaani *role model*. Katika mazungumzo na hawa, wengi wametaja majina mawili makubwa kwenye uandishi wa kisasa; wapo waliosema kuwa *'hadithi za Shigongo zimenifanya nipende kuandika'* . Kwanini wanamtaja Eric Sigongo kama kiigizo kwao?
Sote twajua kwamba Eric Shigongo ni mmiliki wa wa kampuni ya Global Publishers na kupitia magazeti yake ya 'udaku' alikuwa akiweka hadithi zake humo. Sote tutakuwa mashahidi wa jinsi gani hadithi zile zilikamata mioyo na hisia za watu hasa vijana wa kike kwa kiume.

Na wengine hawakusita kusema *'Hussein Tuwa, uandishi wake umenifanya nitamani kuwa kama yeye…'*
Ni zama hizohizo za Eric Shigongo ambapo Hussein Tuwa au kama wengi wanavyopenda kumwita kwa lakabu ya 'Bingwa wa Taharuki' naye kalamu yake ilikuwa kwenye Gazeti la 'udaku' la KIU.

Kwanini wengi wamewataja hawa wawili? Ni kwa sababu hawa waliibuka na kuvunja ukimya mkubwa ulioigubika fasihi ya Kiswahili baada ya miamba kama Agolo Andulu, Alex Banzi, Ndyanao Balisidya, Ben Mtobwa, Elvis Musiba, Dadi Mwawale, Amri Bawji, Eddie Ganzel, Ammie Rajab na wengineo wengi ambao kalamu zao zilitawala miaka ya '80, kunyamaza.
Ni katika hii asilimia 20 ndipo napata kalamu zenye miandiko inayofanana kidogo na hao niliowataja. Lakini kwa asilimia 100 waandishi wote niliozungumza nao ni wazi kwamba kwanza walikuwa wasomaji na usomaji ule ukaibua mwandishi aliye ndani yao.

Sasa hivi tunashuhudia vitabu vya riwaya kuwa biashara kubwa na inayoshika kasi hapa Tanzania. Nachelea kusema kuwa waandishi nguli waliopo sasa kama Japhet Nyang'oro Sudi, Maundu Mwingizi, Mzee Beka Mfaume, Hussein Wamaywa, Goima Mwamigila 'mzee wa Bima ya Penzi', Mohammed Hammie, Laura Pettie, Lilian Mbaga, Vennita Mwita na wengine wengi wamekuwa ni kiigizo kwa waandishi chipukizi wa sasa.

Baada ya kuzungumza mara kadhaa na waandishi hawa, nilihamia kwa wasomaji wa kazi zao. Lengo langu kuu lilikuwa ni kusikiliza wasomaji wanasema nini juu ya wimbi hili la waandishi wa 'kizazi kipya'. Katika tafiti hiyo nilikutana na makundi

matatu ya aina za wasomaji; kundi la kwanza, wengi wao walisema kuwa 'kwa sasa hakuna waandishi kabisa, kazi zote ni mbaya tu hazina viwango kama zile za kina Mtobwa au Musiba' hawa wengi wao walikuwa watu wazima ambao bado wanashindwa kutofautisha nyakati. Kundi la pili, wengi wao walikosoa kazi za sasa eti hazina viwango, wakaenda mbali zaidi wakasema kuwa waandishi hawajui Kiswahili, makosa ya kizembe kama ya sarufi ni mengi, hawajui kutumia R na L n.k. kundi la tatu wao walikuwa hawana mengi, wao wanasoma tu na kununua vitabu.

Niliposikiliza yote haya katika pande zote za fanani na hadhira, ndipo nikagundua kwa nini waandishi wengi hasa wa sasa wanalalamikia soko la vitabu. Labda yaweza kuwa, kuandika kwao bila umakini na kuacha makosa madogomadogo kujitokeza inaweza kuwa ni chanzo cha kupoteza soko la kazi zao.

Binafsi nikaona kwanini niandikie mate wakati wino upo, nikapiga hatua mpaka wanamouza vitabu. Nikanunua baadhi ya vitabu vya waandishi wa ki-sasa, hasa wa riwaya. Naam kile walichosema wasomaji nilikutana nacho kabla hata sijafika kurasa ya kumi ya kila kitabu. Sarufi, muundo, umasikini wa lugha (msamiati), tafiti, uhakika wa lile unaloandika, nyakati na mengine mengi.

***My take...***

Fasihi andishi hususani riwaya, ni uandishi mpana unaohitaji mjumuisho wa mambo mengi sana. Fasihi ni moja ya matawi ya sanaa. Tawi hili hutumia lugha ili kufikisha ujumbe wa fanani kwa hadhira.

Hivyo basi, kama fasihi andishi huwasilishwa kwa lugha basi mwandishi hana budi kuijua lugha hiyo kwa ufasaha. Mwandishi lazima ajue kuwa kuna aina nyingi na tofauti za wasomaji, lakini aina hizo zote zipo kwenye makundi makubwa mawili; wasomaji wa kina na wasomaji wa kawaida.

Hawa wasomaji wa kina ni wale ambao wakishika kitabu chako, watasoma neno kwa neno, aya kwa aya. Hawa huona makosa mengci sana ya kisarufi, makosa mengi sana ya ki-lugha na miundo yake. Hawa ndiwo watakwambia 'waandishi wa siku hizi hamna kitu kabisa'. Huwa hawana haraka ya kumaliza kitabu kwa hii tabia yao. Hawa ni wazuri sana ukiwatumia kama *proof reader* wa kazi yako kabla hujaichapa. Halafu hawa wasomaji wa kawaida ndani yao wameganyika sana, inategemea na nini anataka kwenye hilo andiko.

Hawa husoma ili kuburudika au hata kujifunza lakini hawajali umekosea sarufi au sijui hujaunda sentensi sawasawa. Wao wanachotaka ni 'nini wataka kutuambia'.

Hivyo basi, mwandishi kabla hajaingiza kitabu chake kwa walaji yampasa kuzingatia sana lugha na matumizi yake katika andiko lake. Najua kwamba, kuna baadhi ya waandishi ni ngumu kwao kucheza na lugha hii ya Kiswahili. Hii isikufanye uache kuandika. Ndiyo maana kuna wahariri na wahakiki wa kazi za fasihi.

Kama mwandishi unataka kazi yako ya fasihi ikae vizuri ki-lugha na muundo, na kama wewe mwenyewe huna ubobevu katika hilo basi wapatie kazi yako wahariri na wahakiki. Wao kwa utaalamu wao wataipitia na kuondoa makosa yote yanayoonekana.

Nyote mwataka fasihi iwape 'ugali', siku moja mtembee kifua mbele kwa maandishi yenu. Labda uwe kama Paul Coelho, Stephen King, Chimamanda na wengineo… basi kama hiyo ni ndoto ya kila mwandishi, ni budi kuandika kazi iliyo bora sana ili msomaji aone raha ya kuisoma kila wakati.

Tatizo la kutotumia wahariri na wahakiki limekuwa sugu sana kwa waandishi chipukizi, na kama hamjui, hili ndilo lafanya kila uchao mseme 'riwaya hazina soko'.

Lakini je; ni nani anayetakiwa kutengeneza soko la riwaya? Ni wewe mwenyewe mwandishi. Utajitengenezea soko kwa uandishi mahiri, umakini katika kazi yako, kuzingatia viwango vya uchapaji, kutangaza kazi na kuwa mbunifu katika uga wa matangazo. Zaidi ni kwamba usiogope gharama maana. Ukitaka pesa weka pesa.

Msikate tamaa, maana kuandika ni kuandika tena. Na ili kufika mnapotaka, hamna budi kuandika, kuandika, kuandika.

Asante na alamsiki!

SALUM MAKAMBA

# USHAIRI NI BAHARI SI KIJITO - 02 -

**Sehemu ya Pili**

Baada ya kueleza katika sehemu ya kwanza (toleo lililopita) lengo la kuandika makala hizi, sasa katika sehemu hii ya pili tutazame ikiwa ni kosa kuuita utungo shairi kisa tu umezidi idadi fulani ya beti.

Kuna washairi kwa utashi wao na mitazamo yao huwa wamekubaliana kuwa na sifa kadha wa kadha katika tungo zao. Katika makala ya kwanza nilieleza namna ambavyo Prof. Nabhany pamoja na watunzi wengine wa Lamu, Pate, Siu na baadhi ya sehemu za Mombasa walivyokubaliana sifa za utungo ambao WAO watauita ushairi. WAO. Nasisitiza hapo kuwa ni WAO ili ieleweke kuwa makubaliano ya watu fulani hayapingwi lakini abadani hayapaswi kugeuzwa kuwa ni sheria ambayo kila mshairi sharti aibebe.

Kwa mfano, katika makubaliano ya Prof. Nabhany na wenzake. Waliweka sheria kuwa ili utungo uitwe shairi sharti uwe na sifa zifuatazo;

1. Utungwe kwa bahari moja tu.
2. Uwe na mishororo minne.(4)
3. Uwe na kina na mizani. Kila kipande kati ya ukwapi na utao kiwe na mizani nane (8).
4. Uwe na lugha ya kiufundi, kimafumbo si lugha nyepesi.
5. Ili usichoshe na usikose wa kuusoma beti zake ziwe baina ya moja hadi kumi na mbili. Zisizidi hapo.

Kwa mantiki hiyo, yeyote ambaye angelitunga utungo usio na sifa hizo, basi Prof. Nabhany na wenzake waliokubaliana wasingeliuita utungo huo shairi abadani.

Sasa ajabu ni kwamba, kuna watu ambao katika makubaliano hayo hawakuwepo. Wameyadandia na kuanza kulazimisha watu kuwa ndiyo SHERIA ZA USHAIRI WA KISWAHILI. Ukiwauliza sababu wanasema kasema Prof. Nabhany. Sawa kasema lakini katika kusema kwake kaweka wazi kuwa yalikuwa ni makubaliano ya watu kadhaa. Wao wajibu wa kuyafanya kuwa ndiyo sheria na kanuni zinazopaswa kufuatwa na kila anayetunga wameutoa wapi? Ukiwauliza wanaanza kusema eti unataka kubishana na Profesa. Una elimu ya kubishana naye? Na kadhalika. Hawana sababu za maana.

Na watu hawa ndiyo walionipopoa kwa kusema ati sijui chochote kwenye ushairi, naunajisi ushairi, napaswa nipigwe viboko na niende kujielimisha kuhusu ushairi. Kisa tu nilisema kuwa nimetunga SHAIRI lenye BETI 100 lililo na mishororo minne. Kwa fikra zao utunzi wa namna hiyo haupo na haupaswi kuitwa shairi kwa sababu haukidhi vigezo vilivyowekwa na Prof. Nabhany na wenzake.

Nikataka niwape shule ni wapi nilipopata ruhusa ya kutunga utungo wa namna hiyo na kuuita ushairi. Wakakaza vichwa. Nikasema nitaelimisha watakao kujifunza. Wasiotaka watabaki na ufinyu wao wa fikra.

Ukurasa wa 10 na 11, katika kitabu cha Kunga za Ushairi na Diwani Yetu (1979) kilichoandikwa na Prof. M.M. Mulokozi pamoja na Prof. KK Kahigi unasema, "Hakuna muundo au miundo maalum ambayo lazima ivaliwe na kila shairi, au sheria maalum ZISIZOTANGUKA ambazo lazima zikaririwe na kila mshairi kama 'Sala ya Bwana."

Kwa maneno hayo hadi hapo ni wazi kuwa kulazimisha watu kuwa makubaliano ya watu fulani ndiyo Sheria na Kanuni za Ushairi ni makosa. Kwa hiyo mtu anaweza kutunga tofauti na walivyokubaliana Prof. Nabhany na wenzake na bado alichokitunga kikawa ni shairi.

Katika kurasa hizohizo pia 10 na 11, Prof. Mulokozi na Prof. Kahigi wanaendelea kusema, "Kanuni kuu ambayo kila mtungaji wa shairi yabidi aitimize, kanuni ambayo ndiyo roho ya mashairi… na roho ya fasihi kwa ujumla ni kwamba, muundo wa shairi lazima uamuliwe na kufungamana na mawazo, mtiririko wa hisia, na makusudio ya mtunzi."

SALUM MAKAMBA

## USHAIRI NI BAHARI SI KIJITO -

Yaani mtunzi ndiye ana mamlaka ya kuamua muundo wa shairi lake uweje ili uweze kufikia makusudio ambayo yeye anayalenga. Kwa hiyo kama mtunzi anataka kutunga shairi lenye beti 80 ndipo afikie kusudi lake hakuna kinachopaswa kumzuia. Yeye ndiye anaamua. Kinachotakiwa tu ni kwamba muundo huo ufungamane na mawazo pamoja na mtiririko wa hisia katika kulifikia kusudi lake.

Katika ukurasa wa 29 wanazuoni hao nguli wanaendelea kusema, "Kila mshairi apewe uhuru wa kutumia fani inayofungamana vizuri zaidi na maudhui yake, uwezo wake, na pia hadhira aliyokusudia."

Kwa maelezo hayo, Prof. Nabhany na wenzake walikuwa sahihi kwa kuweka sifa za utungo ambao wao wangeliuita shairi kwa sababu yawezekana ndizo zilikuwa zinafungamana na maudhui, uwezo na hadhira waliyokuwa wameikusudia.

Kwa hiyo leo hii mimi kama nina maudhui yanayohitaji nimwagike beti za kutosha sipaswi kuwekewa ukomo wala kuchaguliwa bahari ya kutumia. Mimi kama mshairi ndiyo naamua kutokana na aina ya maudhui, uwezo nilionao pamoja na hadhira ninayoikusudia.

Hivyo, utungo wenye beti 100, 200 na hata 1000 unaweza kuwa shairi.

Kama hatukupata chanjo za Kifaduro utotoni tujitahidi tupate ili mambo mepesi kama haya tuwe tunayaelewa badala ya kukubali kukaririshwa na kuona wengine hawajui.

*Itaendelea...*

Muhimu:

**Endelea kujipatia Diwani iliyoshinda Tuzo ya Afrika mwaka 2022/23, Mamangu Nipe Wosia pale TPH Bookshop Posta jijini Dar es salaam.**

Wasiliana na;
+255787558448
+255742556446
ili kujipatia nakala yako.

## KAMPENI YA 'CHAFUA DUNIA KWA VITABU VYA KISWAHILI'

Hii ni kampeni iliyo chini ya mtandao wa APE ikiongozwa na Balozi wa APE Majidd Mswahili. Kampeni hii imeanzia huko Ujerumani ambako Balozi huyo wa APE amekabidhi Hidaya tatu tukufu kwa Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani Hassan Mwamweta. Tazama picha hapo chini…







# MSALITI - 05

Na. Richard Mwambe

*Ilipoishia…*

***Kona Lounge ilimpokea Amata dakika kumi na tatu zilizofuata. Nje ya Lounge hiyo palijaa magari ya kila aina. Ungeyaona tu ungejua eeeeenh hapa ni pa wazito. Aliegesha pikipiki yake na kuingia ndani. Humu Amata hajawahi kuingia pamoja na uzururaji wake wote hapo mjini.***

*Endelea…*

Haikumchukua muda kukutana na mwenyeji wake, Mr. Mukhsin. Wakachukuzana pembeni na kuketi.

"Niambie kijana!" Mukhsin akaanzisha mazungumzo.

"Nina shida, kuna simu moja naifuatilia, sasa nataka nijue imepigwa kutoka wapi!" Amata akamwambia. Mukhsin Shashi alikuwa mtu wa makamo, kwa umri wa Amata labda angemwita mzee huyo 'Baba Mdogo'. Mzee huyu mbobevu katika masuala ya mawasiliano aliajiriwa na serikali kwenye shirika la *Dar-Com* tangu enzi za Posta na Simu. Yeye ndiye aliyekuwa mtu wa kutoa ruhusa kama hizo, yaani kufuatilia simu za watu na kadhalika.

"Unataka hilo jambo sasa hivi?" akamuuliza Amata.

"Ikiwezekana, lakini kama itakubidi kutoka kwenye starehe zako basi tulifanye kesho," Amata akajibu.

"Hapana, wala sina haja ya kutoka, kuna mtu pale ambaye atakuhudumia… tena ni mwanadada mremo si ajabu atafurahi kukupokea kijana jamali kama wewe!" Mukhsin akaongea kilevilevi huku akimtania Amata.

"Sawa, fanya hivyo!" Amata akamwambia yule mzee. Mzee Mukhsin akaenda kando kidogo na dakika tatu baadaye akarudi mezani alikomwacha Amata.

"Nenda anakusubiri!"

"Asante!"

"Ukifanikisha usisite kunijuza…" akakazia wakati wanaagana. Amata akaondoka zake kuelekea kwenye mtambo unaorekodi simu zote zinazoingia na kutoka. Hapo palikuwa na *Server* kubwa na ya kisasa iliyokuwa ikifanya kazi hiyo. Jengo la *Extelecom*, ghorofa ya tisa ndipo chumba hicho kilikuwapo. Amata aliwasili na kuchukua kambarau hadi ghorofa husika. Naam alipokelekelewa na mwanadada mweupe, mrefu, mwenye mwili wa wastani.

"Karibu sana, naitwa Faida…" akajitambulisha.

"Naitwa Jaffari!"

"Karibu sana Jaffari, Mukhsini amenipa ujumbe wako, hivyo nilikuwa nakusubiri," Faida akamwambia Amata huku wakiendelea kutembea kuelekea kwenye kile chumba maalum, "samahani, japo huku haruhusiwi kuingia mtu lakini kwa wewe ruksa!" akamwambia Amata huku akifungua mlango uliotengenezwa kwa *aluminiam* tupu na kuingia naye ndani.

"Nashukuru sana maana si kila mtu anaweza kupewa ruhusa ya kuingia kila mahali," Amata akamwambia huku akiketi katika kiti kidogo.

"Enhe, nakusikiliza…" Faida akasema wakati tayari mikono yake imeshaelekea baobonye la kompyuta yake.

"Yeah, nataka nijue namba ya simu iliyopiga kwangu saa mbili na dakika tano usiku… imetoka wapi na ni ya nani?" Amata akamwambia yule mwanamke.

"Nitajie namba!"

"Nikutajie wakati mi ndo nataka uniambie…"

"Hujanielewa kaka, namba ya simu yako ya nyumbani," Faida akamwelewesha mgeni wake.

"Anhaaa ah! Samahani mrembo!"

Neno 'mrembo' lilileta kitu kipya akilini na moyoni mwa Faida. Ni kama vile lilimtekenya mwili mzima na kumfanya amwangalie kijana huyo kwa jicho pembe. Halikuwa jicho la kheri bali lile la kutokupenda utani wa namna hiyo, ingawa lilikuwa na mguso wake.

"02227…" Amata akamtajia.

Baada ya kutajwa namba hiyo ndipo Faida akabofyabofya kwenye Kompyuta yake kisha akasubiri kidogo. Dakika mbili baadaye, akamgeukia Amata akiwa amepata la kusema naye, maana alipomwita 'mrembo' hakutoa jawabu hata la kushukuru wajihi alioumbiwa.

"Namba iliyokupigia ni ya mkoa wa Kagera, nimejaribu kui*trace* vizuri inaonekana ni Ngara!" Faida akamweleza Amata kwa utulivu.

*Ngara!* Amata akawaza, huku akili ikimsaliti kwa kutokuwa na kumbukumbu zozote kuhusiana na Ngara kwa wakati huo. Lilikuwa jambo geni lililomjia bila hodi wala feni ya kumpunguzia kiwango cha joto mwilini mwake.

"Unaweza kumtambua mmiliki wake?" akauliza.

"Innocent Jonathan Kabelwa!" Faida akajibu.

"Innocent Jonathan Kabelwa… ok! Jina si geni sana, ila sikumbuki nimelisikia wapi," Amata

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

akaridhika.

Faida akampa karatasi ndogo iliyoandikwa ile namba iliyompigia, mkoa na jina la mmiliki. Akaipokea na kuisoma, kisha akamtazama yule mwanamke, "mbona yako hujaweka… nikiwa na swali nimfuate tena Mukhsin?" Amata akauliza. Faida akainyakua ile karatasi na kuandika namba yake ya simu akamkabidhi. Jinsi alivyonyakua karatasi ile utadhani wawili hao walikuwa na kisirani.

"Upige ukiwa na shida ya kikazi tu siyo kwa ujinga mwingine!" Faida akasema kwa sauti thabiti.

"Jamani… haya asante kwa kila kitu," Amata akamwambia huku akimkabidhi noti tatu za shilingi elfu kumikumi. Faida hakuzipokea noti zile, ndiyo kwanza akamkazia macho makavu Kamanda Amata na kuanza kuzungumza.

"Mi nimefanya kazi yangu pesa ya nini? Asante sihitaji!" Faida akamwambia Amata huku akiwa wima.

"Sijawahi kuona mwanamke anakataa pesa looh!" Amata akasema na kuzitua mezani kisha akaondoka zake. *Akitaka aziache, akitaka achukue!* Akajisemea moyoni huku akitoka nje ya ile ofisi.

Moja kwa moja akaiendea kambarau na kuteremka chini. Akachukua pikipiki yake na kuondoka eneo hilo huku kichwani mwake kukiwa na mambo matatu tu; Besta, Innosent Jonathan Kabelwa, Ngara. Haya yote inabidi yashughulikiwe haraka iwezekanavyo. Saa tano usiku ilimkuta nyumbani kwake, hakutaka kabisa kujishughulisha na habari ile. Akajitupa kitandani na kuuchapa usingizi.

❦

Walibaki wakitazamana, hawakuwa na la kuzungumza kati yao. Huyu bwana Mkalimoto hata alisahau kuvua sare zake za Jeshi. Alihisi kuchanganyikiwa. "Unajua kupoteza wanajeshi kumi na sita si jambo dogo!" akamwambia yule aliyekuwa naye pale sebuleni. Ilikuwa sebule kubwa iliyokutanisha watu hawa wawili wenye vyeo vikubwa jeshini; Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi (CDF) na Mkuu wa mafunzo.

"Inatafakarisha!" CDF akamjibu.

"Yatupasa kufanya uchunguzi wa kina kuhusu hili… miili kumi na sita lakini miwili haijatambulika kabisa kwa jinsi ilivyoungua," Mkuu wa mafunzo akaeleza.

Tanzania ilikuwa ni moja ya nchi ambayo ilipeleka wanajeshi ishirini na sita katika misheni ya kulinda amani huko Kivu, Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Eneo lenye mapigano yasiyokoma kati ya majeshi ya serikali na waasi wa CRA.

"Tunafanyaje?" akauliza Mkuu wa majeshi.

"Inabidi kutuma watu wakafanye uchunguzi… hapa MI lazima tuwatumie…" mkuu wa mafunzo akaeleza.

"Mimi! Mimi! Mimi…" CDF akatamka huku mkono wake wa kuume akijigusa kifuani kila alipotamka 'Mimi' "…nitume tena watu wangu kule Jehanam! Labda mtu aamue kwenda mwenyewe lakini siyo kwa amri yangu!" akamalizia kusema na kujiegemeza kitini huku mkono wa kuume ukisizumbua nywele zake kwa kuzisukuma kwenda mbele na nyuma.

"Sasa tutafanyaje? Maana kwa vyovyote Rais atataka kujua hatua tunayochukua…"

"Najua, na nitamjibu hivihivi… hata kama atakasirika na kuamua kunivua wadhifa wangu, nitamjibu hivihivi…" akameza funda la mate na kuendelea, "Sana sana nitamshauri tuombe vyombo vya uchunguzi kutoka nje ya nchi," akahitimisha jibu lake.

Mazungumzo ya wawili hawa yalichukua kama nusu saa hivi. Walipotahamaki giza lilishaanza kutafuna nchi, wakaagana na kila mmoja akaondoka zake.

Itaendelea...




Kitabu MSALITI kipo madukani, jikamatie nakala yako kwa Tsh 15,000 tu.

Tembelea duka la Kona ya Riwaya Kinondoni au piga

**simu namba 0655428085**
**Whatsapp 0766974865**

Jikamatie nakala yako sasa

MTUNZI: ASHA SIRAJ
Whatsapp 0789044345



**UTANGULIZI**

**Mapenzi sio kitu cha kuwekea maanani sana kwasababu ipo siku yanaweza kukuletea shida huko mbeleni, kuna baadhi ya changamoto nyingi hutokea. Hivyo ukisema kila jambo uliwekee maanani basi mapenzi yako yatabaki kuwa na majuto siku zote. Kutana na binti SHAZMA aliyepitia mateso mengi kwenye mapenzi yake na kujikuta akijutia kwanini amkabizi moyo wake mwanaume asiye na fadhira**

***Ilipoishia…***

***Kutokana na mwili mnene niliokuwa nao basi nilioneka mkubwa japo sikuwa mkubwa miaka kumi na nne niliyokuwa nayo mtu angeniangalia kwa umakini angezania nina miaka kumi na sita hivi***

*Endelea…*

Siku zilisonga mbele na majibu yalitoka, hivyo nikafaulu na kuchaguliwa kujiunga *form one* kwenye shule ya Sekondari Kalalayoyo na kwa bahati mbaya nilichaguliwa kwenda bweni. Kwa upande wangu ilikuwa furaha kubwa sana
Maana maisha ya pale kwa shangazi ndio *bye bye* . Nilijihisi kunenepa gafla, hakika Mungu ni mkubwa nyie! Yani nilihisi kama ni ndoto hivi.

Kwa upande wa shangazi asingeweza kunizuia kwa sababu alihisi furaha baada ya kujua kuwa naenda bweni, hivyo alihisi kama katua mzigo kwangu akidhani ananikomoa pasipo kujua hata mimi ninayo furaha kwenda kusomea huko
Hata Munira pia alifahuru ila kila mmoja alichaguliwa shule yake Ni mwezi wa kumi na mbili sasa, mume wa shangazi yangu alininunulia vifaa vya shule pamoja na baadhi ya nguo na vitu vingine kipindi hicho nilikuwa nishaanza kuingia kwenye siku zangu, hivyo alininunulia kila kitu hakutaka kabisa nihangaike, kutokana na nidhamu niliyoionesha kwa mume wa shangazi hivyo alikuwa ananipenda sana.

Siku ya mimi kuwasili shule iliwadia niliandaa mizigo yangu na kumuaga shangazi yangu aliyekuwa ukumbini akiangalia tivii.
"Shangazi!" nilimwita, ila hakuonekana kuitikia, mimi sikujali niliendа kukaa karibu yake nikajaribu kumuaga kwa ustaarabu, ila yeye alibaki kunitazama tu bila kunijibu
Nilijikuta nashikwa na hasira kana kwamba naongea na kisiki cha mgomba au, najua hutaki kunijibu ila naelewa nini unakiwaza kwenye akili yako.
Shangazi alinijibu kwa kejeli sana, ni kwamba wewe upo kwenye akili yangu, hata sijui nini umefuata hapa unadhani mimi ninashida yakutaka kuagwa na wewe, ila najua unachokisubilia hapa, umekuja kuniomba pesa alafu unajifanya kujinyenyekea hapa.
Shangazi mimi sio, sio nini? Siuseme tu shangazi naomba pesa, kiufupi mimi sina pesa ya kukupa na mimi sio mtu wakusaidia maskini unanilewa.

Wakati akiongea maneno hayo mume wake alikuwa anasikia kila kitu bila yeye kujua kama mumewe alikuwa amejibanza sehemu hivyo aliongea alivyotaka yeye,
Nilinyanyuka pale kuelekea chumbani kwangu kwa ajili ya kubeba begi langu la nguo pamoja na tranka la kuhifadhia vitu vyangu.
Sauti ya kelele ilisikika ukumbini haikuwa sauti ya mwingine bali alikuwa shangazi yangu.

Baada ya anko Jamary kuondoka basi niliyaanza maisha yangu mapya nikiwa pale shule.
Siku zilizidi kusonga mbele ila nilijikuta naanza kuzoea maisha yale hivyo sikuona tatizo, nilipenda sana maisha ya *boarding* kuliko kule kwa shangazi, japo tulikuwa tunakula ugali kwa sana ila mimi sikujali kabisa, kikubwa niwe na furaha tu
Sijui mambo ya kula ugali usiku na mchana hayo sikuyawekea maanani, niliwekeza akili yangu kwenye masomo yangu ili huko mbeleni na mimi niweze kuwa na ajira yangu

Hivyo nilijitahidi kusoma kwa bidii sana ili niweze kufikia malengo.

***

Ni mwaka wa pili sasa toka niwe hapa shule, anko jamary alikuwa mtu wa kunikumbuka mara kwa mara ila sijawahi kumuona shangazi akija kunitembelea pale hata kusema kukose njia, sikuwahi kumuona.
Roho yangu ilikuwa inauma, ukweli ni kwamba shangazi hakuwahi kunipenda hivyo aliishi na mimi tu ilimradi.

Miezi ilisonga mbele na miaka ikapita. Ni miaka mitatu sasa sikuwahi kufikiria kwenda kumtembelea shangazi kwa sababu niliamini kabisa atakuwa na kisasi na mimi.
Likizo watu walikuwa wanaondoka nyumbani kwao kwenda kuwatembelea wazazi ndugu na jamaa ila mimi maisha yangu yalikuwa ya pale siku zote. Nilitmani sana kwenda ila sikuwa na jinsi.
Kikubwa anko wangu alikuwa anajali kuhusu mimi. Siku moja, ilikuwa siku ya Jumapili mimi pamoja na rafiki yangu judithi tulipanga kwenda kununua baadhi ya vitu.
Ilibidi tukaombe ruhusa kwa *matron* kwa ajili ya kwenda kununua baadhi ya vitu na siku hiyo anko hakuwa nasiku nyingi amenipatia pesa, hivyo pesa nilikuwa nayo, nashukuru alinilipia hada ya shule kama ipasavyo.

Wanafunzi wengine walikuwa kwao, hicho kilikuwa kipindi cha likizo wanafunzi waliobaki pale walikuwa wachache sana. Matron alitukubalia japo aliomba tuwahi kurudi.
Niliondoka mimi pamoja na rafiki yangu Judithi naye hakuwa na wazazi kama mimi hivyo hatukuwa na tofauti tulijua uchungu wa kuwapoteza wazazi.
Wakati tukitoka nje ya geti kuelekea duka moja hivi kubwa kulijaza kila kitu mle ndani, nakumbuka tulikuwa tumevaa nguo za nyumbani.
Tulipendeza sana, hata tulipopata basi walituangalia sisi, tulitumia dakika kumi kufika sehemu tulipokuwa tunaenda
Hivyo tulisogea hadi pale dukani nakuagiza kile ambacho nilikuwa nakihitaji sikumsahau kumnunulia rafiki yangu zawadi, nilimnunulia nguo za ndani pamoja na vitabu, Judithi alishukuru sana kupata rafiki kama mmi.
Hivyo alinikumbatia kwa furaha sana. Nakusema Mungu ambariki sana shazma kwa sasa wewe ni kama ndugu yangu familia yangu, sina familia nyingine zaidi yako.

Nilifurahi sana kusikia maneno mazuri kama hayo, nilijikuta namkumbuka mdogo wangu, ila niliamua kupotezea nilihisi wenda naweza kuipoteza furaha ya rafiki yangu.
Tukiwa tumesimama zetu pale dukani mara alikuja kijana mmoja hivi makamu kama miaka 28 hivi alitutazama pale jinsiw tulivyokuwa tunapiga stori za Uzini.
Alisimama pale dukani na kuagiza kile alichokihitaji. Habari zenu warembo aliongea mwanakaka huyo. Tuliitikia ila hatukumuwekea maanani
Nilishangazwa sana kumuona akinitazama kwa umakini hadi nilijikuta nainamisha kichwa changu chini kwa aibu
Tuliondoka pale tukamuacha akiwa anaagiza mazagazaga yake, Judithi aliniomba tutembee tembea hivyo hatukuwa na kazi ya kufanya huko shule.
"Judithi unajua kabisa matron ametuambia tuwahi kurudi, alafu unaanza mambo yako ya kuanza kupanda je siku ya pili tukimuomba na akatukatalia tutakimbilia kwa nani?"
"Vyovyote vile" alijibu Judith huku akitaka kuvuka barabara kuelekea upande wa pili.
"We jibu hivyo ila siku ya pili tukikataliwa tusianze kulaumiana"
"Ni sawa tu" alijibu Judith huku akitazama huku na kule kama kumepungua magari ili aweze kuvuka. Katika shangaa shangaa zangu Judithi alivuka barabara na kuniacha mimi nikishangaa pale. Niliogopa sana, na kuanza kujiuliza ni vipi nitavuka hapa. Magari yalikuwa ni mengi sana kama unavyojua barabara za Dar es salaam zilivyo, nilibaki kushangaa pale kwa upande wangu nilikuwa bado mshamba wakuvuka barabara kubwa kama hizo.
Sauti ilisikika pembezoni mwangu ikiniomba kunivusha niligeuka haraka nakutaka kujua ni nani huyo anayeniomba kinivusha barabara, Mungu wangu alikuwa kijana yule tuliyemuacha dukani kwanza nilibaki nimeduwaa huku roho yangu ikienda mbio.

*Itaendelea...*



*Endelea...*

Wakati mwingine Khalid alikwenda kwenye duka la Khoja Hussein na wakati mwingine Khoja Hussein alikwenda kwenye duka la Khalid na kuzungumzia mambo mbalimbali yahusuyo vitambaa vya hariri na mazulia na kuhusu wateja wao.

Siku moja, wakati Khoja Hussein amemtembelea rafiki yake Khalid katika duka lake la mazulia, kulikuwa na mtu mwingine pale dukani. Alikuwa akizungumzia kuhusu kununua zulia jipya kwaajili ya nyumbani kwao. Khoja Hussein akamuangali yule mtu kwa umakini kabisa. Alikuwa na uhakika kabisa kwamba huyo mtu ni yule adui yake, Alibaba!!! Kisha Khoja Hussein akaondoka pale dukani haraka sana. Hakutaka Alibaba amuone.

Siku iliyofuata, Khalid alimtembelea Khoja Hussein dukani kwake.

"Yule mtu aliyekuja kukuona jana," alisema Khoja Hussein. "Anafanana sana na rafiki yangu. Alikuwa nani yule?"

"Yule ni baba yangu, Alibaba," Khalid alijibu.

Baada ya hapo wote wakaenda kupata chakula cha jioni katika hoteli kubwa iliyoko maeneo ya pale mjini kama kawaida yao.

Jioni moja, wakati Khalid na Khoja Hussein wakiwa katika matembezi yao mjini pale, Khalid akasimama nje ya nyumba moja kubwa yenye mlango wa bluu.

"Hii ni nyumba ya baba yangu," Khalid alimwambia rafiki yake. "Hapa ndipo tunapoishi. Nimemuelezea baba yote kuhusu wewe – duka lako, vitambaa unavyouza vizuri na upole wako na ukarimu wako kwangu. Anataka kuonana na wewe."

"Ni mkarimu sana, Khalid," Khoja alijibu. "Lakini huenda baba yako akawa na kazi nyingi sana jioni hii."

"Hawezi kuwa na kazi nyingi kiasi cha kushindwa kumkaribisha rafiki yangu kipenzi," Khalid alijibu.

Kisha akafungua mlango na kumkaribisha Khoja Hussein ndani ya nyumba yao. Alibaba alipomuona mgeni yule, alitabasamu na kumpa mkono. "Karibu sana nyumbani kwangu," alisema kwa ukarimu. " Kijana wangu aliniambia mambo yote kuhusu wewe," aliendelea kusema. "Najua wewe ni muuza vitambaa vya hariri muhimu sana hapa mjini na pia ni rafiki mkubwa kipenzi wa mwanangu. Yeye ni kijana mdogo bado na anahitaji kujifunza mengi sana kuhusu mambo ya ulimwengu huu. Wazee kama sisi tunahitaji kuwaongoza vijana hawa katika njia nzuri."

Khoja Hussein aliinamisha kichwa chake kisha akajibu. "Kijana wako ni kijana mzuri sana, na ninafurahia sana mazungumzo yetu, matembezi yetu na pia tunapopata chakula pamoja. Lakini nina uhakika wewe ni mtu mwenye kazi nyingi sana, Alibaba. Ninaondoka sasa ili niwaache wewe na familia yako mkiwa wenye amani."

Alibaba alimshika mkono. "Tafadhali bado usiondoke," alisema. "Ningependa tukae hapa kwa muda huu ili tupate chakula cha jioni pamoja mimi, wewe, Khalid, mke wa Kassim na mke wangu. Marjane yuko jikoni anaandaa kuku mkubwa sana na ataweza kututosha sote."

"Nashukuru sana kwa kunikaribisha," alijibu Khoja Hussein. "Lakini nina tatizo kubwa sana. Siwezi kula chakula chochote chenye chumvi."

Alibaba aliposikia hivyo, alishangaa sana. Ni ajabu sana kusema hivi!!

Alibaba akafikiria kwa muda mfupi, kisha akajibu. "Sawa, hilo halina tatizo. Nitamwambia mfanyakazi asiweke chumvi katika chakula chetu cha jioni leo."

Kisha Alibaba aliendа jikoni na kumkuta Marjane.

*Itaendelea...*



# TUZO YA SAFAL YA FASIHI YA AFRIKA: WATANZANIA WANG'ARA TENA

**Na Mwandishi wetu**

Tuzo ya Safal ya Fasihi ya Afrika msimu wa 2024-2025 ilifikia tamati Julai 3 mwaka huu. Ni ukumbi wa Maktaba mpya ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam uliobeba mamia ya wanafasihi na wapenda fasihi kutoka Tanzania na nje yake.

Hii ilikuwa siku adhimu kabisa kwa wanafasihi walioshiriki katika kinyang'anyiro cha uandishi katika msimu tajwa hapo juu kujinyakulia vitita vyao. Jumla ya Shilingi za Kitanzania Milioni 15 zilitolewa kwa washindi wa kwanza na wa pili katika utanzu wa Riwaya na Ushairi.

Watanzania wang'ara tena katika tuzo hizi zinazoandaliwa kila mwaka. Tuzo hizi zilizoanzishwa mwaka 2014 na Dr. Lizzy Atree na Mukoma wa Ngugi zilikuwa zikiitwa Tuzo ya Kisahili ya Mabati Cornell ya Fasihi ya Afrika.

Ni miswada 350 iliyotumwa kweye kinyang'anyiro hiki na 210 pekee ndiyo ilikizi vigezo vya kutupiwa macho na majaji. Miswada hiyo ilikuwa katika tanzu tatu; riwaya miswada 82, ushairi miswada 116 na hadithi fupi miswada 5 na pia zilikuwapo hadithi kwa picha.

Orodha fupi ilitangazwa na Meneja wa kampuni ya mabati ya Alaf Limited Bi. Hawa Buyuni palepale katika ofisi zao na waandishi bunifu kadhaa walialikwa kusikiliza.

Tangu kuanzishwa kwa tuzo hii tumeshuhudia Watanzania wengi waking'ara kila mwaka, baadhi yao ni; Enock Maregesi, Hussein Wamaywa, Dotto Rangimoto *(Mara mbili),* Salum Makamba, Zainab Bahroon, Lelo Mmasy, Khalfan Sudi na wengine wengi.

Lakini labda inaweza kuwa tofauti na miaka hiyo yote, mwaka huu Watanzania wanne wamenyakua tuzo zote za riwaya na ushairi. Mayassa Abdala riwaya 'Kitanzi cha Mauti' alitangazwa kuwa mshindi wa kwanza na kujinyakulia kitita cha Dolari za Kimarekani 5,000 na Ally Masoud, riwaya 'Nyaraka za Wafu' alitangazwa mshindi wa pili na kujinyakulia kitita cha Dolari 2,500 za Kimarekani. kwa upande wa ushairi ni Bashiru Abdallah, diwani 'Bure Ghali' alitangazwa mshindi wa kwanza na kujitwalia Dolari 5,000 na Mohamed Idrissa, diwani 'Laana ya Uovu' alijitwalia Dolari 2,500.

Kitendo cha Watanzania kujinyakulia nafasi zote kinatupa picha kuwa sasa fasihi ya Kiswahili ina mizizi na matawi hapa Tanzania kwani hii ndiyo lugha ya Taifa.

Lakini tunaona wazi kuwa Tuzo ya Safal ya Fasihi ya Afrika ni moja ya shindano linalowaibua wanafasihi kutoka kule walikojificha na kudhihirisha kwamba uandishi ni ajira, uandishi ni mtaji.

Ngurumo ya Mwandishi tunawapongeza washindi wote na kutoa wito kwa waandishi kutozipuuzia fursa kama hizi, kwani faida yake si 'kitita' tu bali kujulikana kimataaifa na kupata marafiki wapya.



Picha ya pamoja: Washindii watano waliosimama na wageni muhimu, waliokaa.

# HISTORIA YA VITABU ULIMWENGUNI—04

*Na Mwandishi wetu...*

Baada ya Kitabu cha Wafu cha Watibetan (*The Tibetan Book of the Dead)*, ambacho ni maandiko ya kidini na ya kiroho ya ajabu kutoka Tibet kuhusu mchakato wa kifo na kuzaliwa upya, kuna vitabu vingine muhimu ambavyo vina nafasi kubwa katika historia ya vitabu duniani kutokana na athari zao za kiutamaduni, kifalsafa, au kidini.

Hapa chini ni baadhi ya vitabu muhimu vinavyofuatia au kushindana na umuhimu wa kitabu hicho katika historia ya mwanadamu:

1. The Egyptian Book of the Dead (Kitabu cha Wafu cha Wamisri)

Asili: Misri ya kale (karibu 1550 KK).

Maudhui: Maelekezo ya kiroho kwa roho za wafu ili kupita salama kwenye ulimwengu wa wafu na kufikia maisha ya milele.

Umuhimu: Kitabu hiki ni sawa na kile cha Watibetan kwa sababu zote mbili zinahusiana na maisha baada ya kifo. Ni mojawapo ya maandiko ya kale zaidi ya kidini duniani.

2. Bhagavad Gita

Asili: Uhindi (karibu 2,000–2,500 miaka iliyopita).

Maudhui: Mazungumzo kati ya Arjuna na Krishna kuhusu wajibu, roho, kifo, na maisha ya kiroho.

Umuhimu: Moja ya maandiko makuu ya Uhindu; lina athari kubwa kwa falsafa, dini na maisha ya kiroho duniani.

3. Tao Te Ching – Laozi

Asili: Uchina (karibu karne ya 6 KK).

Maudhui: Mafundisho ya taoismu juu ya maisha ya maelewano na asili (Tao).

Umuhimu: Kitabu cha msingi katika falsafa ya Taoismu; kimeathiri sana maisha ya kiroho ya Asia ya Mashariki.

4. Divine Comedy – Dante Alighieri

Asili: Italia (karne ya 14).

Maudhui: Safari ya kiroho ya binadamu kupitia kuzimu (Inferno), toharani (Purgatorio), na peponi (Paradiso).

Umuhimu: Ni mojawapo ya kazi kubwa kabisa za fasihi ya dunia, na ina uhusiano wa kipekee na maisha ya baada ya kifo.

5. The Quran / Biblia / Torah

Asili: Mashariki ya Kati.

Maudhui: Maelezo ya maisha, kifo, maadili, na maisha ya kiroho.

Umuhimu: Vitabu hivi ni vitakatifu katika dini kubwa tatu za Abrahamu – Uislamu, Ukristo, na Uyahudi – na vimeathiri historia, siasa, na maisha ya kiroho ya mabilioni ya watu.

Ikiwa tunafuata muktadha wa maandiko ya kiroho yanayohusiana na maisha ya baada ya kifo au safari ya kiroho, basi Kitabu cha Wafu cha Wamisri kinafuatia kwa karibu sana na kinachukuliwa kama "jamaa" wa karibu wa Kitabu cha Wafu cha Watibetan.

**Kuanzia toleo lijalo tutapitia vitabu hivio kimoja baada ya kingine.**

# MPATANISHI

**NASOMA MPATANISHI…**

*Ameandika Daruweshi Mkulu wa Nyika…*

Alivyoniumba Mungu mimi ni msema kweli na daima mkweli huchukiwa na wengi.
Nitasema kweli daima uwongo kwangu mwiko.
Napenda kusoma ,muda wangu mwingi katika siku hutumika kwenye kusoma hata katika kazi zangu rasmi zote tatu zinazoniingizia kipato asilimia kubwa nikiwa huko huwa nasoma na kuandika sababu sehemu kubwa ya utendaji wakazi hizo unahitajia hivyo.

Baada ya kumaliza kusoma EPA kitabu kizuri kilichotungwa na kuandikwa kiustadi na ndugu yangu Hussein Wamaiywa nimekamata nakala ya Mpatanishi cha Richard Mwambe.
Richard Mwambe ama Kamanda Amata ni miongoni mwa waandishi mahiri sana wa simulizi za kijasusi.
Mwanzoni hata mimi nilihisi huyu jamaa nishushu kweli namna anavyozifungua choza *(code)* za mambo ya ndani .

Nimekuwa nikifatilia kazi zake kwa muda mrefu tangu enzi za Tufaa Jekundu pasi na yeye kujua kama ilivyo ada yangu kujifunza kimyakimya na kutafiti kupitia maandishi ya watu wengine .
Napenda namna ya uwasilishaji wake wa matukio lakini si hivyo tu Richard Mwambe huumba wahusika wanaoishi kweli katika fikra na nyoyo za wasomaji. Wahusika wake hujengwa wakajengeka kihistoria, hisia, misimamo na hata katika migogoro ya ndani inayowahusu .
Kila mhusika ana sauti yake, na hata wale wahusika wadogo nao hawasahauliki. Hii ni sifa ya juu sana kwa mwandishi, kwani si wote huweza kuwafanya wasomaji wamkumbuke hata mhudumu wa mgahawa aliyeonekana mara moja tu katika ukurasa wa pili wa kitabu.

Ukienda katika upande wa maudhui Mwambe habahatishi. Huchota kutoka kwenye uhalisia wa jamii, historia, siasa, dini, mapenzi, na mizozo ya kiakili inayomkumba binadamu katika uhalisia unaoendana na mukhtadha husika.
Si hayo tu zaidi Mwambe ni fundi wa lugha. Anapotumia Kiswahili, hufanya maneno yawe mithili ya sauti ya kinanda,yakicheza na akili ya msomaji kwa uhalisia na ufasaha. Matumizi yake ya tamathali za semi, tashbihi, udamisi, nahau, methali na jazanda huonesha uhodari wake wa lugha ya Kiswahili fasaha lakini si fasaha tu bali iliyo hai. Lugha yake haichoshi, sababu anajua atumie neno gani katika pahala gani na wakati gani.

Ukwasi wake wa lugha unafanya msomaji asikinai kusoma alichoandika.
Anampangilio wa kipekee wa matukio.
Siku zote ili riwaya iwe nzuri, muundo ni kila kitu. Mwambe analijua hilo, na kwa sababu hiyo, hutengeneza muundo wa matukio ambao ni thabiti, wa kuvutia, na usiobeba mapungufu. Anajua pa kuanzisha migogoro, pa kuweka kilele cha mvutano, na pa kumwachia msomaji pumzi kwa suluhisho. Anaweza kutumia muundo wa kurudi nyuma (flashback) kwa ustadi mkubwa.

Kwa unyumbulifu wake na mapito yake ya ajabu hutufundisha kuwa hadithi si kusimulia tu, bali ni sanaa.

Mwambe ni hodari wakuteua mandhari hai .
Mandhari katika kazi za Mwambe huwa si mapambo tu, bali ni sehemu ya simulizi. Ana uwezo wa kutufanya tuone milima, tuhisi joto la jangwani, tusikie kelele za soko, na hata tunuse harufu ya udongo inaponyesha mvua. Ana uwezo wa kipekee wa kuziamsha hisia tano za msomaji kwa wakati mmoja.

Mwambe haandiki kwa mazoea. Kila kazi yake ni tofauti na nyingine. Anabuni baada ya kutafiti jambo linalofanya aibue mambo mapya yaliyofichikana kila siku.
Binafsi nampongeza kwa umahiri wake wa uandishi na njia yake aliyoamua kuitumia ya kuuza baadhi ya kazi zake mtandaoni ili wateja wake tupate kuzisoma kazi zake.

Masimulizi yasiyoeleweka na hadithi za kuokoteza zingine zote mpya nimetupa kule, naendelea kusoma Mpatanishi nishibishe ubongo, nikimaliza nahamia kwa Nadia wa Jane Davis Mwanizuwa Tabora....
#Kusoma siachi n'go.
#Sisomikujionesha nasoma kuelimika..
Mawasiliano: Richard Mwambe
WhatsApp / call 0766974865
Facebook @Amata Ric

**DARUWESHI MKULU WANYIKA MWENESESEME NOGAYA WA SABA (VII)**
**MAGOMENI MWEMBECHAI, DAR ES SALAAM**



Mwenyekiti wa UWAVITA, Bi. Anna Mbise akiwa na Waziri wa Ustawi wa Jamiii, Jinsia na

Balozi wa APE Majid Mswahili akikabidhi kwa Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani moja Hiaya tatu ikiwa ni kampeni maalum ya CHAFUA DUNIA KWA VITABU VYA KISWAHILI.






Hussein Tuwa mwandishi wa kitabu MTUHUMIWA (kulia), akiwa pichani na mmoja wa wasomaji wake katika viwanja vya Sabasaba kwenye Book Signing Day.

Eva Mrema akiwa na mfano wa kitabu cha Mkwe wa Jaji Mkuu kilichozinduliwa katika maonesho ya Sabasaba tarehe 5 Julai.




TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.
Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.
Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com

## NAKUONA MOYONI

Nakutafuta si kwa macho ya nyama,
Bali moyo, penzi lenye heshima,
Kila pumzi ni wimbo wa jina lako,
Ukiwa mbali, nakusikia kwa karibu.

Mapenzi si maneno ya kinywani tu,
Ni matendo ya kufa na kupona tu,
Nikushikapo mkono kwa imani,
Hata dunia hutetemeka, u wangu mwandani.

Nilipoanguka uliniinua bila hukumu,
Ukayafuta machozi yangu kwa tabasamu,
Sauti yako ni tiba ya majeraha,
Mcho yako ni kama taa isiyonipa fadhaha.

Kama mwezi na nyita za usiku,
Umeling'arisha penzi kama wimbo wa chiriku,
Hakika wewe ni baraka isiyo na doa,
Zawadi ya mbingu, kwako, hakuna wa kunitoa.

Naamini tulikutanishwa ka majaaliwa,
Penzi letu ibada, si shairi la tuchawa,
Ukweliwo waninyung'unya rohoni,
Kama moto wa milele, kamwe, hauwashwi kwa kuni.

Twene pamoja bila kurudi nyuma,
Kumshinda hasidi, majaribu na tamaa,
Kwa uthabiti kuwa nimeushika moyo wako,
Nitalilinda penzi hili, mimi na wewe, sako kwa bako.

Kwa jina lako moyo wangu hudunda,
Kama ngoma ya shangwe mbele ya umati,
Mapenzi yako yamenifanya kuwa mshairi,
Kila beti ni heshima ya upendo wako wa dhati.

***AI na Amata Ric***

## KUKATA TAMAA MWIKO

Jambo limekutatiza, usoni jasho meloa.
Akili yako umiza, uweze kujikomboa.
Ubunifu kwako giza, washindwa hata toboa.
Upatapo changamoto, kukata tamaa mwiko.

Kizembe ndugu sideke?, pambana iwe isiwe.
Mwenyewe fanya makeke, sisubiri saidiwe.
Kwanini sasa bweteke?, na wataka fanikiwe.
Upatapo changamoto, kukata tamaa mwiko.

Lazima uwe makini, ndoto zako kutimia.
Dhana waiona chini, umeshindwa itumia.
Utafika juu lini?, shughuliki metulia.
Upatapo changamoto, kukata tamaa mwiko.

Tamaa mimi sikati, japo mwili umechoka.
Nina yangu mikakati, shimoni humu kutoka.
Dongo nalirusha kati, kwa ngazi nitaondoka.
Upatapo changamoto, kukata tamaa mwiko.

Dhana yangu mkononi, taratibu sina pupa.
Na tabasamu usoni, tumaini sijatupa.
Subira yangu moyoni, tapata japo mfupa.
Upatapo changamoto, kukata tamaa mwiko.

Ndiyo maisha si lele, wengi watoa shutuma.
Tuweze kusonga mbele, tukazane kujituma.
Ubunifu si kelele, shimoni tusije kwama.
Upatapo changamoto, kukata tamaa mwiko.


©Jane Davis Mwanizuwa


**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**










Jenga tabia ya kusoma vitabu kila upatapo muda. Vitabu vyetu vinapatikana

Duka la Kona ya Riwaya Kinondoni - Simu namba 0655428085
Posta Mpya Dar es salaam karibu kabisa na mzunguko wa Sanamu ya Askari kwa Joji - Simu 0713454152
Morogoro Morena hotel, Stendi ya Dalala Smaki Samaki na Bima kwa Markus Mpangala - Simu 0719226293
Au wasiliana nasi Jamvi la Simulizi kwa Whatsapp Namba 0766974865

# KUTOKA MAKTABA:MAISHA NI MAPAMBANO—10

**Hiki ni kitabu kilichoandikwa miaka mingi sana nyuma. Kiliandikwa ili kiweze kusomwa na watu mbalimbali na kuwekwa kwenye maktaba za vijijini. Tunakitoa kutoka kwenye maktaba yetu ili kukupa uhondo, Ngurumo ya Mwandishi ni kisima cha fasihi chenye hazina iliyotukuka.**

## TAMAA YA UTAJIRI WA HARAKA HARAKA—9

Tulitaka tupewe jibu la kutosha na kutuondoa shaka kutoka kwake. Mwenzetu akawa na dharau, ikabidi tutafute njia nyingine. Suala kubwa lilihusu mtama wa shamba la shule yetu ulipotelea mahali pasipojulikana.

“Kamati ya kujitegemea ya watoto ilikuwa ikitumaini kwamba mtama huo ungewafaa kwa mlo wa mchana pale shuleni. Kwa sababu watoto wengi walikuwa wanatoka mbali na shule.

Jitihada yetu ya pili ilikuwa ni kumwita mhusika katika kikao rasmi. Hoja ilipotolewa, kikao kilipata mshangao. Mwenzetu huyu ambaye kila mara tulikuwa tukishiriki akageuka na kuwa mtu mwingine kaabisa. Kwanza alieleza kwa taratibu kabisa. Kila mmoja akawa anatumaini kupata ufumbuzi mzuri.

Baada ya kupewa nafasi, alishukuru kwa fursa ile. kisha akahamaki na kutuambia kwamba kwa vile elimu yetu wote tuliohudhuria kikao ilikuwa ndogo, hakuweza kufahamu njia ya kutusaidia! Haukuwepo muda wa kumuuliza ukubwa wa elimu yake ni katika nini na udogo wa elimu yetu ilikuwa na kiini gani. Suala lilihusu upoteaji wa mtama wa watoto wetu. Hatukuelewa uhaba wa elimu yetu ulihusiana vipi. Akaendelea kufoka: ‘Kuwaje mvunje masomo kwa ajili ya jambo dogo kama hili? Mwenyekiti Mama Koroboi akatumia busara zake zote alizokuwa nazo, ili kufahamu jambo la kukosekana kwa mtama.

Kwa kweli mwenyekiti alijitahidi sana. Alikuwa kama mtu ambaye hakusikia lugha chafu ya yule mwalimu. Lakini wajumbe wengine walikwishau dhika sana. Ama kwa hakika siku ile shetani mbaya alikuwa na yule ndugu yetu mwalimu mkuu. Mara akamrukia mama Koroboi, mwenyekiti wetu. Mimi niliporuka kwenda kuamua, mmoja wa walimu alinigonga kisogoni na rula kubwa ya ubao. Nikazirai. Nilipozinduka nikajikuta niko korokoroni. Pale ndani tulikuwa wajumbe wa mkutano. Siku ya pili tukabanwa pingu imara na kuongozwa kwenda mahakamani. Ukiniambia nisahau siku ile sitakubali hata kwa nini. Kwa bahati mbaya tena mimi nilifanywa kuwa mshtakiwa wa kwanza. Mashitaka yakiwa kunzisha fujo na kuhatarisha amani kwa jumuia. Kulikuwa na watu ambao sikuwafahamu waliofika kutoa ushahidi wa uwongo. Sote tuliyakataa mashitaka. Shauri liliendesha kwa majuma mawili. Siku ya hukumu ikafika. Hakimu alizungumza kwa kifupi isivyo kawaida. Akamalizia kwa kusema; “Kutokana na ushahidi uliotolewa hasa ule wa Mzee Likongo, ni vigumu kwa washitakiwa kuingia hatiani. Hivyo nawaachia huru kutoka muda huu’ akatulia kidogo, kisha akaendelea: ‘Kwenu mlio huru sitasita kupokea mashitaka dhidi ya walalamikaji waliowashitaki’. Akamaliza. Mambo yakageuka, washitaki kuwa washitakiwa”.

Matokeo ya mkasa huo ni kwamba mpaka muda huu mwalimu mkuu, Mzee Panya na mwalimu mmoja bado wanaendelea kutumiakia vifungo vyao vya miaka miwili kila mmoja. Pamoja na adhabu hiyo, wakitoka walipe fidia kwa shule na kwamba baada ya kifungo mwalimu panya awe anapewa maadili kutoka wizara ya afya na ustawi wa jamii kwa muda wa mwaka mmoja.

Pamoja na mkasa huo shule na kijiji kwa ujumla havikuteterekа. Maendeleo yalizidi kusonga mbele.

Mpepo hakuridhika na hatua aliyofikia yeye binafsi. Aliwahimiza wanakijiji wengine—hasa mke wake Sofi na pia Mzee Likongo ambaye ni mzee kuliko wote. Alitumia mbinu nyingi pamoja na methali kadha wa kadha. Methali aliyoipendelea ni ile isemayo “Lisilo na mkono nujikonalilo” - maana ya methali hii ni kwamba jaambo lolote baya ambalo halina wa kulimaliza basi hujimaliza lenyewe. Lakini papo hapo Mpepo alikuwa hakubaliani na methali hiyo hasa kuhusu ujinga wa kutokujua kusoma na kuandika. Yeye alikubaliana na methali nyingi nyingine kama vile “Asiyefunzwa na wazazi hufunzwa na ulimwengu”. Au asiyesikia la mkubwa huvunjika…… hayo yote ni mabaya ambayo hujitatua yenyewe. Lakini siyo ujinga!

***Itaendelea toleo lijalo….***

# ELIMU JAMII

## SAFARI YA MALEZI – 2

**1.1 NAFASI YA WAZAZI KATIKA MALEZI**

Wazazi ni mwanga wa kwanza katika maisha ya mtoto. Kabla hajakutana na jamii, shule au marafiki, huanza kwanza kujifunza dunia kupitia macho ya baba na mama. Hapo ndipo msingi wa malezi hujengwa, sio kwa maneno maneno tu, bali kwa uwepo wa kweli, kwa mfano wa maisha, na kwa upendo unaojitoa kila siku.

Kazi ya mzazi si kazi ya kawaida. Ni wito wa kipekee wa kushiriki na Mungu katika uumbaji wa utu. Kwa njia ya malezi yao, wazazi wana nafasi ya kuumba mioyo yenye hekima, nafsi zilizo imara, na roho zinazojua kupenda. Kila hatua ya mtoto, kila neno lake la kwanza, kila kosa lake dogo, vyote vinahitaji jicho la mzazi, jicho linalotazama si kwa hukumu, bali kwa neema.

Katika kipengele hiki, tutaangalia jinsi nafasi ya mzazi inavyokuwa nguzo ya malezi, tukianza na mchango wa baba, kisha mama, na hatimaye ushirikiano wao kama mzazi mmoja wa familia, wakifanya kazi kama moyo mmoja kwa ajili ya ukuaji mzima wa mtoto.

Mwandishi

KELVIN KYARA

**1.1.1 Malezi ya Baba kwa Mtoto**

Baba ni kama nguzo katika safari ya malezi, ana nafasi ya kipekee ambayo haiwezi kuzibwa na mtu mwingine yeyote. Mtoto anapomtazama baba, anajifunza juu ya ujasiri, nidhamu, msimamo, na namna ya kumtazama Mungu kama Baba wa milele.

Baba hulea kwa mtindo wa kimya-kuangalia.
Kuangalia ni sehemu ya kwanza ya malezi ya baba, angalia mwenendo wa mtoto wako, sio kwa kumtafutia kosa, bali kwa kutambua mwelekeo wake. Kwa sio kila kosa mtoto analiona.

Baba mwenye hekima hamfanyi mtoto aogope kusema ukweli, bali humwelekeza kuona kuwa kusema kweli ni kujiheshimu. Anamwonyesha mtoto kuwa uaminifu ni msingi wa uhusiano wowote mzuri, na kuwa hata akikosea, bado anaweza kurekebisha mambo kwa kusema ukweli.

Baba anapaswa pia kujifunza kumsikiliza mtoto wake kwa makini, hata kama mazungumzo ni ya kitoto. Kupitia usikivu wa baba, mtoto hujifunza kuwa mawazo yake yanathaminiwa, na kuwa yuko huru kueleza hisia zake. Katika kusikiliza, baba hupata nafasi ya kugundua kinachomsumbua mtoto kabla hakijawa tatizo kubwa.
Malezi ya baba hayahitaji pesa nyingi, bali moyo wa kujitoa. Mtoto hataikumbuka sana zawadi aliyopokea, bali atakumbuka baba aliyemshika mkono alipokuwa naogopa, baba aliyemchekea alipohisi kukataliwa, baba aliyemwombea alipokuwa usingizini. Huo ndio uzito wa nafasi ya baba katika malezi, kazi ya kupalilia moyo wa mtoto kwa hekima, upole, na uthabiti.

**1.1.2 Malezi ya Mama kwa Mtoto**

Mama ni uso wa kwanza mtoto anaoona mara anapozaliwa. Ndani ya uso huo kuna dunia nzima ya maana, faraja na usalama. Ni kupitia uso wa mama ambapo mtoto huanza kuelewa lugha ya upendo hata kabla hajajua kuongea.
Katika safari ya malezi, mama hubeba sura mbalimbali, kila sura ikiwa na wajibu maalum katika kumlea mtoto kuwa binadamu kamili.

**1.1.3 Nyuso mbalimbali za mama katika malezi**

**Mama kama Mlezi wa Haraka (Fast Responder)**

Mama husikia kilio cha mtoto hata kabla wengine hawajakielewa. Yeye husikia sauti ya kimya, huona kilichojificha haraka. Anaweza kuamka usiku wa manane kwa milio midogo tu, na kwa upole hushughulikia hitaji lolote. Huu ni uso wa utayari—mtazamo unaosema "nipo kwa ajili yako," hata bila maneno.

**Mama kama Mpatanishi (Modulator)**

Katika nyakati za vurugu au hali za hisia kali, mama huja kama mto wa utulivu. Huonyesha mtoto jinsi ya kutuliza hasira, kukubali kushindwa bila kuvunjika moyo, na kuelezea huzuni bila kuogopa. Uso wake hutuliza dhoruba, na sauti yake huongoza mtoto kurudi katika hali ya utulivu wa ndani.

**Mama kama Kioo (Mirror)**
Mtoto hujifunza kumtambua mwenyewe kwa kuangalia kwenye uso wa mama. Anapotabasamu, mtoto hujifunza kuwa yeye ni wa thamani. Anapopokea hisia zake bila hukumu, mtoto hujifunza kujikubali. Mama humrudishia mtoto picha ya nani alivyo na thamani yake, hata kabla hajaitambua mwenyewe.

**Mama kama mchakataji wa hisia (Processor)**
Wakati mwingine mtoto haelewi anachohisi. Anaweza kulia, kukasirika, au kuvurugika bila sababu anayoielewa. Mama huja kama mfasiri wa hisia. Humuuliza: "Una huzuni kwa sababu...?" au "Labda umechoka?" Hiyo humsaidia mtoto kuanza kuelewa ulimwengu wa ndani na kujenga ujuzi wa kihisia.

**Mama kama msimulizi (Storyteller)**
Katika simulizi za mama kuna hekima, historia, utambulisho, na maadili. Anaposimulia hadithi, anaweka ndani ya mtoto mbegu ya ndoto, ujasiri, na huruma. Hadithi za mama huishi katika moyo wa mtoto hata baada ya miaka mingi, zikimwelekeza katika maamuzi makubwa ya maisha.
Katika sura hizi zote, mama hubaki kuwa uso wa upendo wa Mungu ulio karibu kabisa na mtoto. Katika tabasamu lake, mtoto huona tumaini. Katika macho yake, mtoto huona hatima. Katika mikono yake, mtoto hujua maana ya kupendwa, kulindwa, na kulelewa.
Mama si mtu wa kawaida, ni zawadi ya kila siku, baraka ya maisha, na mwalimu wa upendo wa kweli.

**1.1.3 Malezi ya wazazi wote kwa pamoja**
Malezi bora hayajengwi na upande mmoja tu wa mzazi. Ingawa baba ana nafasi yake ya kipekee, na mama ana sura zake muhimu, kuna nguvu ya ajabu inayojitokeza pale wanaposhirikiana. Malezi yanapobeba sauti mbili, moyo wa pamoja, na lengo moja, mtoto hujengwa kwa utimilifu wa kiakili, kihisia, kiroho, na kimwili.

Mtoto anapokua katika familia ambamo baba na mama wamesimama pamoja, hujifunza uzito wa ushirikiano, maana ya mshikamano, na uzuri wa upendo wa kweli. Wazazi wanapozungumza kwa sauti moja kuhusu maadili, nidhamu, upendo, na imani, mtoto hujenga msimamo thabiti. Wakati wazazi wanapotofautiana hadharani au kukosoana mbele ya mtoto, moyo wake hupasuka vipande viwili. Lakini wakishikamana, hata katika tofauti zao, mtoto hujifunza kuwa upendo unaweza kushinda kila changamoto.

**1.1.4 Athari ya malezi ya mzazi mmoja.**
Malezi ya mzazi mmoja, hasa inapomkosa mzazi wa jinsia tofauti, yanaweza kumwathiri mtoto kihisia na kijamii. Msichana anayekua bila baba hukosa mfano wa upendo wa kiume, jambo linaloweza kumletea changamoto katika ndoa. Vivyo hivyo, mvulana asiyelelewa na mama hukosa upendo wa kike, na huenda akapata ugumu wa kuelewa jinsia hiyo. Kukosekana kwa msingi huu kunaweza kusababisha mtazamo mbaya kuhusu ndoa, kuchanganyikiwa kijinsia, au hata kutafuta upendo kwa jinsia yake kama njia ya kujaza pengo la kihisia. Wengi huingia kwenye ndoa wakiwa na majeraha ya utotoni, jambo linalochangia migogoro na kuvunjika kwa ndoa. Hivyo, ushirikiano wa wazazi wote ni muhimu katika kujenga maisha bora ya baadaye ya mtoto.




- **TANGAZO DOGO KWA SHILINGI 5000 TU KWA TOLEO.**
- **TANGAZO KUBWA 'KURASA NZIMA' KWA SHILINGI 10,000 TU.**

# HAPPY NEW YEAR '07'—Twahir Yusuph

***Ilipoishia...***
***"Sawa, mfuatilie nini anafanya kwa sasa, na mienendo yake." aliongea na kutoa kibunda cha pesa na kumkabidhi Domy. Baada ya jukumu la kwanza kulikamilisha, sasa anapewa kazi ya pili, ni kumfuatilia Labi Kimati.***

Domy alikunja noti zake na kuzitia mfukoni. Akashuka ndani ya gari hiyo ya Inspekta Kasese na kutokomea zake anapopajua. Labi Kimati likawa jina la kwanza kuifanya kalamu ya inspekta Kasese kuutumia wino wake juu ya karatasi. Aliliandika kwa wino mweusi kama binadamu namba moja anayepaswa kumfahamu na kumfuatilia, yeye ndiye pekee aliyeonekana kuwa mtu wa karibu na marehemu wote wawili hadi muda huo, hii iliufungua mlango wa kesi yake inspekta Kasese.

Kwenye kundi la marafiki watatu, wawili wanafariki kwa kufuatana! Tena vifo vya kufanana! Mmoja anabaki hai! Wasiwasi wake wa kwanza ukasimama hapo. *Kama huyu rafiki yao Labi Kimati hatokuwa anafahamu vyanzo vya kupotea kwa uhai wa rafiki zake wote wawili, basi anaweza kuwa muhusika, au labda asiwe na hatia yoyote.* Aliwaza inspekta Kasese. Huu ulikuwa mwanzo mzuri uliompa mwangaza kwenye kesi yake. Dhima yake ikawa ni kuujua undani wa urafiki wa vijana hao watatu. Kichwani akayabeba maswali mengi, ambayo majibu yake alishapafahamu pa kuyapata.

Hakutaka kuchelewa, muda huohuo inspekta Kasese alimpigia simu mkuu wake IGP Edward Kituo na kuomba kuonana naye, hakuzuiliwa. Dakika chache baadae nyayo zake zikamsimamisha mbele ya mkuu wake huyo kikakamavu, huku mkono wake mmoja ukitoa heshima kwa saluti kama ilivyo kanuni zao. Alimaliza na kukaribishwa kitini Inspekta Kasese.

"Mkuu, nina maswali kuhusiana na marehemu Jax, ambaye ni mwanao, ningeomba ushirikiano wako." Inspekta aliongea.

"Endelea." ruhusa ikatolewa na IGP Edward Kituo, mboni zake zikionesha umakini pajini.

"…Ningeomba kufahamu uhusiano wako ulikuwaje na kijana wako, namaanisha ukaribu mkuu, labda kuwasiliana kwa kupitia simu mara kwa mara, au alikuwa kijana wa aina gani, anapenda nini labda." alisitisha, akimtazama mkuu wake machoni. Aliitusha mikono yake mezani, akavipatanisha viganja vyake, vilishikana. Mboni zake zikawa sambamba na paji la inspekta Kasese.

"Mara nyingi niligombana naye kwa kutotaka kuwa kama mimi baba yake, namaanisha askari polisi." Alianza kuongea IGP Edward Kituo. "Tangu udogo wake ndoto yake ilikuwa kuja kuwa mfanyabiashara mkubwa, alitamani kumiliki kampuni kubwa ya kibiashara. Hakuvutiwa kabisa na kazi ya upolisi." aliweka tuo, kisha akaendelea, "Jax alikuwa kijana mwenye upendo sana, nikiwa kama baba yake nilipambana ili kuhakikisha nasapoti ndoto zake, nilifanya kila ambacho ni sahihi kwa mwanangu, na alikuwa mtu wangu wa karibu sana, tuliwasiliana mara kwa mara."

"Kuhusu marafiki je? Ningependa kufahamu afande.." swali la pili anatupiwa IGP.

"Imraan Rashidi ambaye pia ni marehemu, pamoja na Labi Kimati, hawa ndiyo rafiki, na watu wa karibu wa Jax baada ya familia yake. Waliongozana popote walipokwenda, kama kuachana ilikuwa mara chache sana. "

"Samahani mkuu, siku ya tukio uliwasiliana naye?"

"Ndiyo, ilikuwa jioni. Alinieleza angechelewa kurudi nyumbani, sababu angepitia kwa rafiki yake Labi Kimati baada ya kutoka ofisini kwake ili kwenda kuzungumzia ishu zao za kibiashara." Jina la Labi Kimati likatajwa kwa mara ya pili masikioni mwake, ikisadikika marehemu alikuwa na mpango wa kuonana naye, tena siku ya tukio. Taarifa hiyo ikamvutia mno Inspekta Kasese.

"Walikuwa wanafanya biashara pamoja?" aliuliza Inspekta Kasese.

"Hapana, walikuwa na mpango wao wote watatu, wa kufungua kampuni kubwa ya uzalishaji nguo za kisasa pamoja."

"Unamaanisha pamoja na marehemu Imraan pia?"

"Ndiyo."

"Kwahiyo walikwenda kuonana wote watatu siku hiyo?"

"Ndiyo, bila shaka." Kimya kidogo kikakizonga kinywa cha Inspekta Kasese, taswira yake ilionesha kufikiria kitu.

"Najua unachokiwaza Inspekta, hata mimi kilinitokea, lakini uhusiano na ukaribu wa hawa vijana watatu, ulinitoa shaka juu ya hilo, japo sikuacha kuchunguza."

"Hapana afande, nawaza kingine." ilichopoka kauli ndimini mwa Inspekta Kasese, akimtazama mbonini IGP wake.

"Kiseme Inspekta."

"Nawaza muuaji atakuwa alimteka muda gani Jax, ni baada ya kuonana na rafiki zake au kabla?"

"Imraan na Labi walithibisha wote watatu kukutana, niliwauliza usiku ule, walizungumza mipango yao na kuhitimisha kisha wakaachana. Hivyo muuaji alimteka Jax baada ya kikao chao kutamatika, nadhani akiwa anarejea nyumbani muda huo, maana hakuna pahali angeenda usiku huo bila rafiki zake pamoja, au wao kujua." Akiwa mwenye taswira ya udadisi kimya kifupi kikakishika tena kinywa chake. Tamati akalipata neno.

"Asante afande, nilitaka kufahamu machache kumhusu Jax, na ninashkuru kwa msaada wako mkuu."

"Okay, mi nikutakie kazi njema, kila la kheri Inspekta." aliongea akinyoosha mkono IGP. Alisimama akaupokea inspekta na kutoa heshima mbele ya mkuu wake, kisha akatoweka ndani ya ofisi hiyo.

Alifika nje hadi garini mwake, akili yake ilikuwa ikiyatafakari kwa kina maelezo aliyoyapata kutoka kwa mkuu wake. Aliwaza kuwa bila shaka watu wa mwisho kuonana na marehemu Jax, ni Imraan pamoja na Labi Kimati, na baina yao amebaki mmoja tu. *"Marafiki watatu waongee kuhusu biashara, kisha siku hiyohiyo mmoja afe, siku inayofuata anakufa mwingine tena vilevile kwa kifo cha aina moja! Ajabu mmoja anabaki hai hadi leo? Kwanini hajafa? Au yeye sio shabaha ya muuaji! Hakupaswa kufa labda!"* Aliwaza Inspekta. Alishika kichwa akifanya kama anajikuna, *"Bila shaka napaswa kuzungumza na CDF Rashidi koboko pia, nahitaji kumfahamu Imraan kwa undani."*

Hakutaka siku iishe, wala kuutumia muda mwingi kuendelea kufikiria vitu vigumu anavyopaswa kuvichunguza kwanza. Alimtafuta CDF Rashidi Koboko na kumuomba kumtembelea ili aongee naye machache. Alikubaliwa. Alikaribishwa kambini, ndani ya ofisi ya mkuu huyo wa majeshi ya ulinzi na usalama wa nchi, akiwa bila sare za kipolisi Inspekta Kasese. Vikombe viwili vya kahawa vikiwa mezani, huku viti viwili vikiibeba miili hai ya binadamu hao walio kwenye kikao kifupi. Alikuwa CDF Rashidi Koboko alieyafungua maongezi hayo.

"Karibu sana Inspekta, hapa pia ni nyumbani kwako."

"Nashukuru sana mkuu, nimevutiwa na ukarimu wa pahala hapa." Alitabasamu CDF Rashidi Koboko, kisha akazungumza, "Nipo tayari sasa, niulize chochote." ruhusa ilitoka.


"Samahani mkuu, nilikuwa napenda kumfahamu Imraan, tabia, na hata ukaribu wake na wewe." Tabasamu jingine liliangaza pajini mwa CDF Rashidi Koboko, huku huzuni pia ikionesha kumnyemelea. Huenda alikumbushwa jambo ambalo labda hakutamani kulisikia, lilizifinya hisia zake.

"Alikuwa akiniheshimu sana Imraan, mara nyingi nilihisi faraja kila aliponikimbilia na kunikumbatia muda nilipowasili nyumbani, nauzungumzia utoto wake." aliweka tuo.. "Alipoanza kukua, nilimpa uhuru wa kufanya alichokipenda, na kutembea kwenye ndoto zake, sikumlazimisha achague nilichokitaka mimi, sababu niliamini ni Maisha yake sio yangu."

"Pole sana mkuu, kama nimeuliza swali ambalo halijakufanya ujisikie vizuri."

"Najua upo kwenye misheni ngumu, na unastahili kuuliza chochote sasa kuhusu yeye. Hivyo ondoa shaka inspekta"

*Itaendelea...*



# RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (02)- Na: Eva Mrema

*Ilipoishia...*

***Aliambatana na mimi hadi nje ambapo nililiendea gari langu na kuingia ndani. Nilifunga milango, kisha mkanda. Nilifungua kioo na kumpungia kama ishara ya kumuaga. Niliondoka eneo lile na kuelekea moja kwa moja nyumbani.***

***Endelea…***

Niliishi na mdogo wangu wa kiume, ambaye, ndiyo jukumu pekee nililokuwa nalo baada ya kupoteza wazazi wetu wote wawili kwenye ajali ya meli, miaka mingi iliyopita. Dogo alikuwa chuo. Tulikuwa na utofauti mkubwa wa ratiba, yeye alilala mapema na kuamka kwa kuchelewa, hali ya kuwa mimi nililala kwa kuchelewa na niliamka mapema sana kuwahi kibaruani kwangu.
Tulionana mwisho wa juma kama hakukutokea changamoto iliyohitaji uwepo wangu. Ni kama tuliishi nchi tofauti. Yaani tuliwasiliana kwa simu na muda mwingine barua. Kiukweli nyumbani paliniboa sana. Kutoka ilikuwa kama nafasi yangu ya kukutana na dunia.

Usiku wa kukutana na Sunche ulikuwa wenye hisia mchanganyiko kwangu. Baada ya kuingia ndani, nilikoga na kujipumzisha nilikosa usingizi kabisa. Niligalauka kitandani kwa kugeuka huku na kule.
Sijui ni nini kilinipata.

**SURA YA PILI.**

Usingizi wa alfajiri unaumiza sana, haswa, ukiambatana na ndoto nzuri isiyotamatika. Niliamshwa na kengele niliyoizoea, japo siku hii nilitamani isingetimiza wajibu wake. Nilikurupuka nikajiandaa kama kichaa mwenye shibe. Tabasamu usoni halikunitoroka kabisa. Nilipasha moto maji, yalipopata uvuguvugu nikayatia limao. Niliyanywa mkupuo ili yanipunguzie mning'inio wa ziada.

Nilitoa gimbi kwenye jokofu, nikalipasha kwenye kipashio changu. Nilihifadhi kwenye bakuli linalotunza joto na kuliweka ndani ya mkoba wangu. Nilimtumia ujumbe mfupi dogo, japo tulilala chini ya paa moja. Nilimwachia pesa ya matumizi na kumkumbusha kuwa makini.

Niliondoka giza lingalipo. Mara nyingi nilikimbia mapema asubuhi hadi ofisini na nilifika kabla ya wengine, nilitumia muda huo kujimwagia maji na kujiweka sawa. Ni ratiba ninayoitii kwa miaka sasa. Nafanya mazoezi asubuhi na jioni. Hivyo natoka nyumbani nimevaa nguo za mazoezi na nikifika ofisini nabadilisha. Jioni nafanya vivyo pia, navalia ofisini za mazoezi, na hua nakimbia hadi nyumbani. Napenda mwili wangu uwe imara, napinga magonjwa maana naogopa sana dawa mimi.

Ratiba yangu ilikwenda vizuri. Nilishinda mwenye amani sana. Ni kama tayari niliingia penzini kabla ya kuingia penzini. Wakati natembea kurejea nyumbani, niliutafakari usiku uliopita. Nilijilaumu kwa ujinga mmoja mzuri sana niliofanya. Sikuchukua namba ya simu ya Mzungu.

Niliwaza na kuwazua kisha nikaamua niende kule tulipokutana. Nilifika nyumbani na kabla sijapumzika niliiweka nyumba katika hali ya usafi. Nilitia nguo kwenye mashine ya kufulia kisha nilikosha vyombo alivyovitumia mdogo wangu mchana.
Nilimtumia dogo ujumbe na kumfahamisha nitatoka, hivyo nikamsihi kama alikuwa karibu ajongee tuonane. Niliingia chumbani na kupaweka sawa. Nilizirudia nguo kwenye mashine na kwenda kuzianika. Nilikoga vizuri sana. Nilijipaka mafuta na kisha manukato. Nilijipa dakika kadhaa za kupumzika nikimngojea dogo.
Bwana, bwana! Usingizi ulipotoka kwani napajua? Nililala kama pono. Nilikuja kushituka usiku wa saa nne. Nilikurupuka nilipobaini ndoto yangu nzuri ningeweza kuipoteza baada ya siku hii. Nilitoa nguo kabatini na kuvaa kama nakimbizwa. Asikwambie mtu uongo, ninapendana sana na nguo nyeupe, ukinikosa hapo utanikuta kwenye nyekundu…lakini nyeupe kwangu ndo mapenzi yalipo. Nilivaa gauni jeupe lililoshika mwili vizuri. Nilivaa na raba maana kwa haraka yangu viatu vya wazi vingenichelewesha.

Nilitoka mpaka sebuleni na kumkuta mdogo wangu akiangalia filamu ya Kijapani. Yeye anaitwa Tobiasi jina la babu wa baba yetu. Ni kijana mdogo asiye na furaha kabisa. Alinikazia hata mimi dada yake. Mara nyingi alilaumu juu ya wazazi kutuacha hali tunawahitaji. Nilimwambia hiyo ni mipango ya Rabana. Nilimfuata na kumkumbatia japo hakunionesha ushirikiano kabisa. Nilimuaga na kutoka. Alinikimbilia baada ya mimi kuwasha gari, alinipatia koti lake la jinsi

# RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (02) - Na: Eva Mrema

na kuniambia 'nguo niliyovaa ni nyepesi nivae na koti'. Moyoni nilitabasamu, lakini usoni nilimshukuru kawaida.

Safari ya kwenda baa iliiva. Sikukutana na changamoto maana tayari ilikuwa usiku uliokwiva. Kwa kawaida kuingia kwenye ile baa lazima uwe na kadi au ujisajili. Nilimiliki kadi. Niliitoa na ku-*scan* kisha nilielekea moja kwa moja ghorofani ambako nilikaa jana. Niliangaza huku na kule bila matumaini ya kile nilichokitarajia. Niliagiza mchemsho na kuanza kuunywa. Nilijikuta nikitabasamu kila nikikumbuka mazungumzo yangu na Sunche jana yake.

Muhudumu alikuja, ni mdada aliyekuwa kanizoea kiasi. Tulisabahiana na mwisho alinipasha habari iliyonipa mshtuko mkubwa. Sikuweza kuendelea kula. Sikufanikiwa kuendelea kukaa kochini. Nilinyanyuka kama mshale kwenye tamthilia za kituruki. Nilimkabidhi pesa anilipie mchemsho na kisha nilianza kutoka nje. Mbio hadi garini kwangu, nilikazana kukanyaga moto hali ya kuwa sijawasha injini.

Niliupiga usukani kwa hasira. Niliulaumu usingizi kwa kila kitu.

*"Tabita jitulize! Tulia tafadhali"* nilijiambia. Nilivuta pumzi na kuitoa mara kadhaa. Sauti ya yule dada mhudumu ilijirudia ikifoka mawazoni.

*"Mamii, yule Mzungu ambaye mlikaa wote jana alikuja na kukuulizia. Alikaa sana hapa na mara zote aliniita na kuniuliza kama kweli utakuja ama la! Sikuwa na jibu, nilimtania tu kuwa azingatie nguo nyeupe, pengine angekuona. Nilitoka nje kuzungumza na simu. Niliporejea nilikuta ugonvi, mashangazi wawili walikuwa wakimgombania meneja wetu. Mzungu wako mwenye roho ya huruma, akaingia vitani kuomba amani isiyomuhusu. Bahati yake mbaya chupa iliyolenga kumpiga usoni yule shangazi mweupe mnene ilitua kwenye mkono wa Mzungu na kuishia kumtia jeraha kubwa. Tuliogopa sana, lakini walinzi na viongozi walilibeba jukumu la kumpeleka hospitali, kule St. Constantine".* Nilivuta tena pumzi na kujihoji maswali ambayo sikuweza hata kujijibu. *Huyu mtu ni nani kwangu? Mbona namhofia sana mtu nimekutana naye jana tu? Tabita tulia. Tabita acha mapepe, huyu sio wewe kabisa."* Nilijisihi sana na hatimaye nilipopata afueni ya hali, niliwasha gari kwa usahihi na kwa mwendo wa kawaida niliendesha hadi St. Constantine. Nilitoa maelezo yaliyoeleweka kiasi cha mimi kuruhusiwa kwenda kumuona Sunche.

Tayari alishonwa nyuzi ishirini na moja nyuma ya mkono karibu na kiwiko. Sijui madaktari walisubiri nini kukifunika kidonda kile kilichoniumiza kuliko aliye kibeba. Machozi yalinilenga japo nilijizuia sana kuonesha hisia zangu. Nilimkaribia nikiwa na kimuhemuhe cha kumkumbatia, lakini muuguzi aliingia na kunitaka nisubiri nje amfunge bandeji. Nilimpungia Sunche naye alitabasamu.

Baada ya dakika nyingi za ukarabatiwaji, nilipata wasaa wa kumkaribia. Nilimkumbatia kwa sekunde mia mbili na kumi. Usiniulize nilijuaje, itoshe kusema niliyahesabu mapigo ya moyo wake. Nilimuachia na wote tukachukua nafasi. Niliketi kwenye kiti kando ya msaidizi wake ambaye tulisabahiana kama tumekwisha kuonana. Sikumzingatia kabisa, hata salamu sikumbuki kama nilimpa ya kumfaa. Sunche alimtuma akamchukulie sharubati. Alikuwa akihisi kiu. Nilinyanyuka nikachukue mimi.

"Nakutaka karibu yangu, acha Miso aende" Sunche aliongea na kunikata kiherehere. Niliketi hali nikitabasamu. Miso aliondoka na kutuacha peke yetu. Sunche alinyanyuka kijasiri japo maumivu yalikuwa dhahiri shahiri; akanikaribia, akanitazama weeh! "*Can I hug you Tabita?* Akaniuliza.

Nilihisi raha hadi kwenye unywele wa mwisho.

***Itaendelea...***

**RIWAYA: NGUVU YA KIAPO**

Inapatikana katika kitabu (nakala ngumu) na soft copy (nakala tepe) kwa bei ya kirafiki.

**KITABU** - Tsh 10,000
**Dar es salaam:**

- Duka la Kona ya Riwaya - 0655428085
- Kalamu Tulivu Magomeni - 0718975659
- Posta Mpya kwa Joji - 0713454152
- Temeke kwa Eva Mrema - 0742630141

Soft Copy (Nakala tepe) PDF - Tsh 5,000
'Offer' kupitia Ngurumo ya Mwandishi ni - Tsh 3,000
Lipa kwa **MPESA LIPA NAMBA 36499709 Eva John Mrema**

## Tangazo





www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi
jamvilasimulizi@gmail.com